# MIONGONI MWA ITIKADI ZA MASHIA

‘Abdullaah Bin Muhammad As-Salafiy

## YALIYOMO

**Utangulizi Wa Shaykh ´Abdul-´Aziyz Bin ´Abdullaah Ibn Baaz, Kiongozi Wa Jopo La Wanavyuoni Wakuu Wa Saudi Arabia** .................................................... 4

**Utangulizi** .............................................................................................. 5

**Ni Lini Limedhihiri Kundi La Raafidhwah?** ........................................... 7

**Kwanini Shia Wameitwa Raafidhwah?** .................................................. 8

**Raafidhwah Wamegawanyika Makundi Mangapi?** ................................ 9

**Ni Ipi Itikadi Ya Al-Badaa Wanayoiamini Raafidhwah?** ..................... 10

**Ni Ipi Itikadi Ya Rafidhwah Kuhusu Sifa Za Allaah?** ......................... 11

**Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Qur-aan Hii Tuliyonayo Ambayo Allaah Kachukua Ahadi Ya Kuihifadhi?** ............................................... 13

**Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Maswahaba Wa Mtume (Swalla Allaahu ´Alayhi Wa Sallam)?** .............................................................. 15

**Raafidhwah Wanafanana Na Mayahudi** ............................................... 17

**Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Juu Ya Maimamu?** ................................ 19

**Ni Ipi Itikadi Ya Kurejea Wanayoiamini Raafidhwah?** ....................... 21

**Ni Ipi Itikadi Ya "Taqiyyah" Kwa Raafidhwah?** ................................... 22

**Ni Ipi Itikadi Ya Udongo Wanayoiamini Raafidhwah?** ....................... 24

**Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Ahlus-Sunnah?** ....................... 25

**Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Ndoa Ya Mut'ah Na Ina Ubora Gani Kwao?** ............................................................................................. 27

**Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Najaf Na Karbalaa, Na Je, Kuna Fadhila Gani Katika Kuzuru Sehemu Hizi?** ......................................... 30

**Ni Mambo Gani Ambayo Raafidhwah Wametofautiana Na Ahlus-Sunnah?.** ............................................................................................................. 33

**Ni Ipi Itikadi Ya Raafidwah Kuhusu Siku Ya ´Aashuraa? Na Ina Ubora Gani Kwao?** ........ 34

**Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Bay'ah (Kutoa Ahadi Ya Kumtii Mtawala).** ........ 35

**Ni Ipi Hukumu Ya Kujenga Mahusiano Na Ukaribu Kati Ya Ahlus-Sunnah Na Raafidhwah Washirikina?** ........ 37

**Ni Zipi Nukuu Za Salaf Na Khalaf Kuhusu Raafidhwah?** ........ 38

**Suratul-Wilaayah Ambayo Wanadai Iliondolewa Katika Mus-haf** ........ 43

**Lawh (Ubao) Wa Faatwimah Wanaodai Mashia** ........ 45

**Du'aa Ya Masanamu Wawili Wa Ki-Quraysh - Wanamkusudia Abu Bakr Na ´Umar (Allaah Awawiye Radhi)** ........ 47

**Hitimisho** ........ 48

**Rejea Muhimu Ambazo Tunamnasihi Kila Muislamu Kuzijua Katika Kuwajibu Raafidhwah** ........ 50

**Miongoni Mwa Vitabu Vya Wanavyuoni Wa Zama Hizi** ........ 50

**Tovuti Muhimu Za Kuwajibu Raafidhwah Ithnaa-´Ashariyyah, Ambazo Tunakusihi Uzitembelee** ........ 51

## Utangulizi Wa Shaykh ´Abdul-´Aziyz Bin ´Abdullaah Ibn Baaz, Kiongozi Wa Jopo La Wanavyuoni Wakuu Wa Saudi Arabia

*Kwa jina la Allaah Mwingi wa Rahma Mwenye kurehemu.*

Kutoka kwa ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz, kwa ndugu yangu mkarimu…. Allaah Amuafikishe. Amani ya Allaah iwe juu yako na Rahma Zake pamoja na baraka zake, amma ba'ad:

"Kutokana na barua yako ulioituma kwangu ya tarehe 10/2/1418H kuhusu kitabu chako, juu ya "Mashia", tumekisoma, na kukiona kuwa ni kizuri na muhimu sana, kinafaa kukisambaza hapa Saudia na kwingineko, na tunamuomba Allaah Awanufaishe kwacho Waislamu na Atie baraka katika juhudi zenu. Amani ya Allaah iwe juu yenu na Rahma pamoja na baraka Zake."

**Mufti wa Saudi-Arabia.**

## Utangulizi

Shukrani zote zinamstahiki Allaah peke yake, Rahma na amani zimwendee Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pamoja na ahli zake na Swahaba wake wote.

Amma ba'ad:

Hakika sababu za msingi zilizonipelekea kuandika kitabu hiki na hali iliyojionyesha ya kushamiri kwa harakati za Raafidhwah za kuwalingania watu katika dhehebu hili potofu na harakati hizi zimekuwa kiulimwengu, na kutokana na hatari kubwa ya kundi hili kwa dini ya Uislamu na kutokana na hali ya kughafilika na kujisahau kwa Waislamu wengi kutokana na hatari ya kundi hili, na kutokana na itikadi yao iliyojaa ushirikina, na kuitukana Qur-aan na Maswahaba (Radhi za Allaah ziwe juu yao) na kupituka mipaka juu ya Maimamu wao, ndio maana nimeazimia kuandika kitabu hiki na kuyajibu mambo yanayowatatiza watu kuhusu kundi hili kwa muhtasari, nikufuata nyayo za Shaykh wetu Shaykh ´Abdullaah bin ´Abdir-Rahmaan Al-Jibriyn (Allaah Amrehemu) katika kitabu chake "At-Ta'aliyqaat ´alaa Matni lumu´atil I'itiqaad" na kwa kunukuu katika vitabu vya Raafidhwah ambavyo ni maarufu na mashuhuri kwao, na katika vya Ahlus-Sunnah miongoni mwa wema waliotangulia na waliokuja baaada yao ambao waliwajibu Raafidhwah na kubainisha ubovu wa itikadi zao zilizosimama juu ya ushirikina, na uongo, na kuchupa mipaka, na matusi.

Na nimejaribu kwa kadiri ya uwezo wangu katika kitabu hiki kuwasimamishia hoja, kupitia vitabu vyao wanavyovitegemea, kama alivyosema Shaykh Ibraahiym bin Sulaymaan Al-Jab-haan (Allaah Amrehemu) ***"Nitakusimamishia hoja kupitia mdomo wako ewe Shi'a."***

Mwisho namuomba Allaah Awanufaishe kupitia kitabu hiki wenye mazingatio kama alivyosema Allaah:

"Hakika katika hayo mna ukumbusho kwa wenye kuwa na nyoyo zinazozingatia, au mwenye kutega sikio na hali moyo wake uko haadhwir" [Qaaf 50: 37].

Natoa shukrani kwa kila aliyechangia katika kitabu hiki, namuomba Allaah Awalipe kila la kheri. Rahma na amani zimuendee bwana wetu Muhammad na ahli zake na Maswahaba zake.

Imeandikwa na **'Abdullaah Muhammad As-Salafiy.**

## Ni Lini Limedhihiri Kundi La Raafidhwah?

Lilianza kundi la Raafidhwah wakati alipojitokeza Myahudi mmoja aitwae ´Abdullaah bin Sabai akidai kuwa ni Muislam, na kwa madai ya kuwapenda Ahlul-Bayt (watu wa nyumbani kwa Mtume) na akapituka mipaka katika kumtukuza ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhu) na akadai kuwa Mtume alimuusia kuwa Khalifa baada yake, kisha akamnyanyua na kumuweka katika daraja ya uungu na haya yanathibitishwa na vitabu vya Ki-Shia. Kwa mfano Al-Qummiy katika kitabu chake '*Al-Maqaalatu wal-Firaq'*.[1]

Anakiri kuwepo kwake (Ibnu Sabai) na anamzingatia kwamba ndie mtu wa mwanzo aliyesema kuhusiana na Uimamu wa ´Aliy na kurejea kwake, na akaanzisha kuwatukana Abu Bakr na ´Umar na ´Uthmaan na Maswahaba wengine, kama alivyosema An-Nuubakhtiy katika kitabu chake '*Firaqu Ash-Shi'ah'*. [2]

Na kama alivyosema pia Al-Kushiy katika kitabu chake *maarufu 'Rijaalul-Kushiy'*. [3]

Na katika Mashia wa sasa hivi wanaosema kuwepo kwa ´Abdullaah bin Sabai ni Muhammad bin ´Aliy Al-Mu'allim katika kitabu chake *'´Abdullaah bin Sabai Al-Haqiyqatul-Majhuulah'*. [4]

Na mtu kukubali jambo ndio dalili kubwa, na hawa wote tuliowataja ni katika Masheikh wakubwa wa ki-Raafidhwah.

Amesema Al-Baghdaadiy: "As-Sabaiyyah ni wafuasi wa 'Abdullaah bin Sabai ambae alichupa mipaka katika kumtukuza ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhu) na kudai kuwa alikuwa ni Nabii, Kisha akachupa mipaka zaidi mpaka akadai kuwa alikuwa ni mungu."

Na amesema Al-Baghdaadiy vilevile: "Na alikuwa Ibnu Sawdai yaani Ibnu Sabai - asili yake ni Myahudi katika watu wa Aliirah, akadhihirisha Uislamu kwa kutaka awe na ukubwa kwa watu wa Al-Kuufa, akawaambia (watu wa Kuufa) kwamba amekuta katika Taurati kwamba kila Mtume anaye Waswiy

---

1 *Al-Maqaalaatu wal-Firaq cha Al-Qummiy* uk. 10-21.

2 *Firaqu ash-Shi'ah* cha An-Nuubakhtiy uk. 19-20.

3 Aliyoyataja Al-Kushiy katika riwaya zake mbalimbali kutoka kwa Ibni Sabai na itikadi zake, tazama namba: 170, 171, 172, 173, 174 katika uk. 106-108.

4 Na kitabu hiki ni majibu ya kitabu alichokitunga Mshia aitwae Murtadhwa Al-'Askariy kwa anuani, *'Abdullaah bin Sabai wa Asaatwiru Ukhra'* ambae alipinga katika kitabu chake kuwepo kwa Abdullaah bin Sabai.

(mrithi) na kwamba ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhu) ndie mrithi wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)".

Na amesema Ash-Shihristaaniy kuhusu Ibni Sabai kwamba ndiye mtu wa kwanza aliyesema kwamba kuna nasswi (dalili) juu ya uimamu wa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhu), na akaeleza kuhusu kundi la Sabaiyah kwamba ndilo kundi la kwanza lililoanzisha itikadi ya kutoweka kwa Imamu wao wa kumi na mbili (Al-Mahd Al-Muntadhwar) na kurejea kwake, kisha Shia wakarithi itikadi hiyo baada yao, pamoja na kutofautiana kwa makundi yao, kuhusu Uimamu wa ´Aliy na Ukhalifa (uongozi) wake. Na hayo ni katika athari za Ibni Sabai, na yaliongezeka makundi ya Shia na itikadi zao na kauli zao yakawa makundi mengi sana. Na hivi ndivyo walivyozua Mashia itikadi ya Al-Waswiy, Ar-Rajaa, Al-Ghaybah, bali itikadi ya kwamba Maimamu wao wana sifa za uungu(5) kwa kumfuata Myahudi Ibnu Sabai.

## Kwanini Shia Wameitwa Raafidhwah?

Jina hili kalitaja Shaykh wao Al-Majlisy katika kitabu chake(Bihaarul-Anwaar) akasema katika mlango aliouita, mlango kuhusu (Ubora wa Raafidhwah na uzuri wa kujiita jina hili), kisha akataja kutoka kwa Sulaymaan Al-Aamash kuwa amesema: "Niliingia kwa Abu ´Abdillaah Ja'afar bin Muhammad nikasema kumwambia: Hakika watu wanatuita Raafidhwah, nini maana ya Raafidhwah? Akasema: Wa-Allaahi si wao waliokuiteni hivyo bali, Allaah Alikuiteni hivyo katika Taurati na Injili kupitia ulimi wa Nabii Muwsaa na Nabii ´Iysaa(6).

Na imesemekana kuwa: "Wameitwa Raafidhwah kwa sababu walikuja kwa ´Aliy bin Hassan wakamwambia: Jitenge na Abu Bakr na ´Umar ili tuwe pamoja nawe, akasema: "Wao ni vipenzi wa Babu yangu, siwezi kujitenga nao bali niko pamoja nao"; Wakasema: "Hivyo basi tumekukataa, ndipo wakaitwa Raafidhwah, na akaitwa kila aliyemuunga mkono Zayd kuwa ni Zaydiyyah." (7)

5 *Uswuwl I´itiqaad Ahlis-Sunnah wal-Jama´aah* cha Al-Laalakaaiy 1/22-23.

6 Tazama kitabu *Bihaarul-Anwar* cha Al-Majlisy 65/97 (ambacho ni miongoni mwa marejeo yao muhimu katika vitabu vyao vya sasa).

7 *At-Taaliqaat ´alaa Matni Lum´aatil I´itqaad* cha Shaykh ´Abdullaah Al-Jibriyn uk. 108.

Na inasemekana: “Wameitwa Raafidhwah kwa kupinga kwao utawala wa Abu Bakr na ´Umar.” [8]

Na imesemekana: “Wameitwa hivyo kwa kukataa kwao Dini.”[9]

### Raafidhwah Wamegawanyika Makundi  Mangapi?

Imekuja katika kitabu *‘Daairatul-Ma´arif’* kuwa "Makundi ya Shia ambayo ni mashuhuri yako zaidi ya sabini na tatu"[10]; bali imepokewa kutoka kwa Raafidhwah Mir Baaqir Ad-Daamand[11]kwamba makundi yote yaliyotajwa katika Hadiyth, Hadiyth ya kugawanyika kwa Ummah wa Muhammad katika makundi sabini na tatu yamekusudiwa makundi ya Mashia, na kwamba lililotajwa kuwa ni kundi lililosalimika ni kundi la Imaamiyyah. Na ametaja Al-Maqriiziy kuwa makundi yao yanafikia mia tatu.[12]

Na amesema Ashihristany: "Hakika Raafidhwah wamegawanyika katika makundi matano: Al-Qiisaaniyyah, Az-Zaydiyyah, Al-Imaamiyyah, Al-Ghaaliyyah, Al-Ismaailiyyah."[13]

Na amesema Al-Baghdaadiy: "Hakika Raafidhwah baada ya zama za ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhu) wako makundi manne: Zaydiyyah, Imaamiyyah, Kiisaaniyyah, na Al-Ghulaatu."[14]

Lakini yakupasa kutambua kuwa Zaydiyyah si katika kundi la Raafidhwah ispokuwa ni katika kundi la Al-Jaaruudiyyah.

---

[8] Tazama *Maqaalaatul-Islaamiyiyn* cha Muhyud-Diyn Abdul-Hamiyd 1/89.
[9] *Maqaalatul-Islamiyiyn* 1/89.
[10] *Daairatul Ma'arif* 4/67.
[11] Ni Baaqir bin Muhammad Al-Istiraabaadiy, Maarufu kama Al-Miir Ad-Damaad, amekufa mwaka 1041. Tazama maelezo yake katika kitabu (Al-Kunaa-wal-Al-Qaab) cha Abbaas Al-Qummiy 2/226.
[12] Ni Al-Maqriiziy 2/351.
[13] *Al-Milal wan-Nihal* cha Ash-Shihristaaniy uk. 147.
[14] *Al-Farqu baynal-Firaq* cha Al-Baghdaadiy uk. 41.

## Ni Ipi Itikadi Ya Al-Badaa Wanayoiamini Raafidhwah?

Al-Badaa maana yake ni kudhihiri baada ya kutoweka, au kwa maana ya kuanzishwa kwa rai mpya. Na neno hili (Al-Badaa kwa maana zote mbili linamaanisha kuwepo hali ya kutojua jambo kisha kujua kunakuja baadae, na mambo yote haya mawili kwa Allaah ni muhali. Raafidhwah wanainasibisha sifa hii ya ( Al-Badaa) kwa Allaah.

Imepokewa kutoka kwa Rayyaani bin As-Swalt kwamba amesema: "Nilimsikia Ar-Ridhwaa akisema: Hajapata Allaah kumtuma Nabii yoyote ispokuwa kwa kuharamisha pombe na kukiri (Al-Badaa) kuwa ni katika sifa za Allaah."[15] .
Na kutoka kwa Abdullaah amesema: "Hajapata kuabudiwa Allaah kwa jambo lolote kama Al-Badaa." [16]

Tazama ndugu yangu Muislam jinsi wanavyomnasibishia Allaah sifa ya ujinga. Ilihali Allaah Anasema:

"Hakuna alioko katika Mbingu na Ardhi ajuae Ghaybu (yasioonekana au yasiyojulikana) ila Allaah" [An-Naml : 65].

Badala yake wanaitakidi kuwa Maimamu wao wanajua elimu zote, wala halifichikani kwao jambo lolote. Je, hii inaweza kuwa itikadi ya Uislamu aliyokuja nayo Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)?

15 *Uswuwlul-Kaafiy* uk. 40.
16 *Uswuwlul-Kaafiy* cha Al-Kulayniyiy katika kitabu Tawhiyd 1/331.

## Ni Ipi Itikadi Ya Rafidhwah Kuhusu Sifa Za Allaah?

Raafidhwah ndio watu (kundi) wa mwanzo waliopinga Sifa za Allaah na kudai kuwa kumthibitishia baadhi ya sifa ni kumfanya kuwa ana kiwiliwili. Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah kamtaja mtu wa kwanza kuleta itikadi hii katika Raafidhwah kuwa ni Hishaam bin Al-Hakam[17] na Hishaam bin Saalim al-Jawaliiqiy na Yuunus bin Abdir-Rahmaan Al-Qummiy na Abuu Ja'afar Al-Ahwal.[18]

Wote waliotajwa hapo juu ni katika Masheikh wakubwa wa Ithnaa-´Ashariyyah, kisha wakawa Jahmiyyah wanaopinga Sifa za Allaah, kama vile wengi wao katika riwaya zao nyingi walivyomsifu Allaah kwa sifa mbaya ambazo waliziambatanisha na sifa ambazo zinathibiti kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

Amepokea Ibnu Baabawayhiy zaidi ya riwaya sabini (70) zinazosema kuwa Allaah, "Hasifiki kwa zama, wala sehemu, wala namna, wala kutikisika, wala kuhama toka sehemu hadi sehemu nyingine, wala hana sifa miongoni mwa Sifa za kimaumbile, wala huwezi kumuhisi, wala yeye si kiwiliwili, wala hana sura."[19]

Na kwa hiyo Masheikh wao wakafuata njia hii potofu, pamoja na kuzikataa sifa za Allaah zilizothibiti katika Qur-aan na Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Vilevile wanapinga na kukataa kuteremka kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) katika mbingu ya dunia katika theluthi ya usiku kama ilivyothibiti katika Hadiyth sahihi, na wanasema kwamba Qur-aan imeumbwa (si maneno ya Allaah) na wanapinga kumuona Allaah siku ya Qiyaamah (wanadai hatoonekana).

Imekuja katika kitabu *'Bihaarul-Anwaar'* kwamba Abu ´Abdillaah Ja'afar Asw-Swaadiq, aliulizwa kuhusu Allaah (Subhanaahu wa Ta´ala), je Ataonekana siku ya Qiyaamah? Akasema ametakasika Allaah na hilo kutakasika kuliko

17 *Minhaajus-Sunnah* 1/20 cha Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah.
18 *I´itiqaadaatu Firaqil-Muslimiyn wal-Mushrikiyn* uk. 97.
19 *At-Tawhiyd* cha Baabawayhiy uk. 57.

kukubwa, hakika macho hayaoni isipokuwa kitu chenye rangi na umbile, na Allaah ndiye Muumbaji wa rangi na maumbile.(20)

Bali wamesema, lau kama mtu atamnasibisha Allaah na baadhi ya sifa, kama vile kuonekana, basi anahukumiwa kama ameritadi (katoka katika Uislamu). Haya yamepokewa kutoka kwa Sheikh wao Ja'afar An-Najaafiy.(21)

Lakini ni muhimu utambue (ndugu msomaji wa kitabu hiki) kwamba Allaah Kathibitisha Mwenyewe katika Qur-aan kuwa Waumini watamuona siku ya Qiyaamah kama ilivyo kuja katika Suratul Qiyaamah:

" (Kuna) Nyuso siku hiyo zitakuwa ni zenye kung'ara. Ni zenye kumtazama Mola wao." [Al-Qiyaamah : 22-23].

Na imethibiti katika Sunnah sahihi za Mtume, kama ilivyo katika Swahiyh Al-Bukhaariy na Muslim, katika Hadyith ya Jurayj bin 'Abdillaah Al-Bajaly, kasema: "Tulikuwa tumeketi na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akautazama mwezi usiku wa tarehe 14 akasema:

"Hakika mtamuona Mola Wenu kama mnavyouona mwezi huu, hampati shida katika kuuangalia." (22)

Na Aayah na Hadiyth zinazothibitisha jambo hili ni nyingi hatuwezi kuziorodhesha zote.

[20] *Bihaarul-Anwaar* cha Al-Majlisiy 4/31.
[21] *Kashful-Ghitwaai* ukurasa wa 471.
[22] Al-Bukhaariy 544, na Muslim 633 kwa faida.

## Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Qur-aan Hii Tuliyonayo Ambayo Allaah Kachukua Ahadi Ya Kuihifadhi?

Hakika Raafidhwah, ambao katika zama zetu ndio wanaitwa SHIA/MASHIA wanasema: "Hakika Qur-aan tuliyonayo si Qur-aan ile Aliyoiteremsha Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), bali imebadilishwa, ikazidishwa na kupunguzwa."

Na jamhuri wa Wanavyuoni wa Hadiyth wa ki-Shia wanaitakidi kwamba Qur-aan imebadilishwa, hii ni kwa mujibu wa maneno ya An-Nuuriy Atw-Twabrisiy katika kitabu chake '*Faswlul-Khitwaab fiy Tahriyf Kitaab Rabbil-Arbaab*'.[23]

Na amesema Muhammad bin Ya'aquub Al-Kulayniy, katika kitabu chake '*Uswuwlul-Kaafiy*' katika mlango aliouita, 'Hawakuikusanya Qur-aan yote isipokuwa Maimamu' (anakusudia Maimamu wao wa ki-Shia), kisha akaleta riwaya ifuatayo:

"Kutoka kwa Jaabir, amesema: Nilimsikia Abu Ja'afar akisema: "Hajapata kudai mtu yeyote kuwa kaikusanya Qur-aan yote kama Alivyoiteremsha Allaah ispokuwa atakuwa ni muongo. Hakuna aliyeikusanya na kuihifadhi kama alivyoiteremsha Allaah isipokuwa ´Aliy bin Abi Twaalib na Maimamu baada yake."[24]

Na imepokewa toka kwa Jaabir toka kwa Ja'afar kwamba amesema: "Hawezi kudai mtu yeyote kwamba anayo Qur-aan kamili isipokuwa walioachiwa wasia."[25]

Na imepokewa kutoka kwa Hishaam bin Saalim, toka kwa Abii Abdillaah (Ja'afar) amesema: "Hakika Qur-aan aliyokuja nayo Jibriyl kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni aayah 17,000."[26]

---

23 *Faswlul-Khitwaab* cha Husayn bin Mahdi Taqiyyun-Nuuriy Atw-Twabrasiy uk. 32.
24 *Uswuwlul-Kaafiy* cha Al-Kulayniy (1/228).
25 *Uswuwlul-Kaafiy* cha Al-Kulayniy (1/285).
26 *Uswuwlul-Kaafiy* cha Al-Kulayniyiy (2/634) kathibitisha kwa riwaya hii katika kitabu chake '*Qiraatu al-'Uquul*' (12 525).
Akasema: Hadiyth hii ni thiqa (ya kutegemewa).

Maana ya maneno hayo ni kwamba Qur-aan wanayoidai Raafidhwah ni zaidi ya Qur-aan hii tuliyonayo -ambayo Allaah Kachukua ahadi ya kuihifadhi- zaidi ya mara tatu. Tunamuomba Allaah Atukinge na upotofu wao.

Na ametaja Ahmad Atw-Twabrisiy katika kitabu chake '*Al-Ihtijaaj*' kwamba ´Umar alimwambia Zayd bin Thaabit: "Hakika ´Aliy alikuja na Qur-aan, ndani mna fedheha za Muhajiriyn na Answaar, na tumeonelea tutaje Qur-aan nyingine na tuyaondoe mambo yote ya fedheha za Muhajiriyn na Answaar, Zayd akakubaliana naye katika hilo.

Kisha akasema: Endapo mtamaliza kuiandika Qur-aan kama jinsi mtakavyo nyinyi, halafu ´Aliy akadhihirisha Qur-aan aliyonayo, je, hatokuwa kabatilisha kazi mliyoifanya?. ´Umar akasema: Hivyo ni lipi la kufanya? Zayd akasema: Wewe ndio utajua ufumbuzi, `Umar akasema: Hakuna ujanja zaidi ya kumuua ´Aliy ili tupate kupumua, akafanya mipango ya kumuua ´Aliy kupitia Khaalid bin Waliyd, lakini hakuweza.

Pindi ´Umar alipotawala ukhalifa, alimuomba ´Aliy awape Qur-aan ili waibadilishe, akasema ´Umar: "Ewe Abal-Hassan (´Aliy) Waonaje ungetuletea Qur-aan uliyokuwa umeileta kwa Abu Bakr ili tuwaunganishe watu katika Msahafu mmoja? Akasena (´Aliy) Hakuna uwezekano wa jambo ulitakalo, kwani nilikuwa nimeuleta kwa Abu Bakr ili kunisimamishia hoja na ili msije kusema siku ya Qiyaamah:

"Hakika sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo" [Al-A´araaf : 172] au msije kusema "Haikutujia" [Al-A´araaf : 129], hakika hii Qur-aan hawaigusi isipokuwa waliotwaharika, na wale waliousiwa katika wanangu (kizazi changu). ´Umar akasema: Je, kuna muda maalumu wa kuidhihirisha? ´Aliy akasema: Ni pale atakaposimama mtoto katika watoto wangu akiidhihirisha na kuwaamrisha watu kuifuata. [27]

Na kwa vyovyote vile watakavyojidai Mashia kukikana kitabu cha An-Nuuriy Atw-Twabrisiy, kwa itikadi yao ya 'Taqiyyah', Hakika kitabu hicho kimejaa (kimesheheni) mamia ya dalili toka kwa Wanavyuoni wao katika vitabu vyao tegemezi, zinazothibitisha kwamba wao wanaitikadi na kuamini kuwa Qur-aan imebadilishwa isipokuwa hawapendi kuamsha makelele (na malumbano) kuhusu itikadi yao hii juu ya Qur-aan.

[27] *Al-Ihtijaaj* cha Atw-Twabrisiy, uk. 225, na kitabu *Faswlul-Khitwaab* uk. 7.

Na inabaini kuwa kuna Qur-aan mbili, moja inayojulikana kwa Waislamu wote, na nyingine ni makhsusi (maalumu) imefichwa, na hiyo ndio kunapatikana ndani yake Surat Al-Wilaayah, ambayo Mashia wanadai kwamba iliondolewa katika Qur-aan.

Pia katika Aayah ambazo wanadai kufutwa katika Qur-aan, ni ile aliyoitaja An-Nuuriy At-Twabrasiy katika kitabu chake *'Faswlul-Khitwaab fiy Tahriyf Kitaab Rabbil Arbaab'* ambayo ni: "Na tukainua utajo wako kwa ´Aliy ambaye ni mkwe wako." Wanadai imeondolewa katika Suratul-Inshiraah (Alam Nashrah) wala hawaoni haya katika madai yao haya hali yakuwa wanajua wazi kuwa Surah hii ni Makkiyyah (imeteremshwa Makkah) na ´Aliy hakuwa mkwe wa Mtume Makkah.

## Ni Ipi Itikadi Ya Raafidwah Kuhusu Maswahaba Wa Mtume (Swalla Allaahu ´Alayhi Wa Sallam)?

Imejengeka itikadi ya Raafidwah juu ya kuwatukana na kuwakufurisha Maswahaba wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) Rahma na amani zishuke juu yao.

Ametaja Al-Kulayiniy katika kitabu *'Furuw'ul-Kaafiy'* kutoka kwa Ja'afar "Waliritadi watu wote baada ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) isipokuwa watu watatu; Nikasema: Ni kina nani hao watatu? Akasema ni Miqdaad bin Aswad, na Abu Dhariy Al-Ghifaariy, na Salmaan Al-Faarisiy."[28]

Na ametaja Al-Majlisiy katika kitabu *'Haqul-Yaqiyn'* kwamba mtumishi wa ´Aliy bin Al-Husayn kasema: "Nilikuwa naye (´Alayhis-Salaam) katika baadhi ya sehemu alizokuwa akijitenga, nikasema kumwambia: Hakika mimi ninashakia baadhi ya haki kwako, naomba nieleze kuhusu watu hawa wawili, Abu Bakr na ´Umar, Akasema: Ni makafiri na kila mwenye kuwapenda ni kafiri."

Pia imepokewa toka kwa Abu Hamzah Athumaliy kwamba alimuuliza ´Aliy bin Al-Husayn kuhusu Abu Bakr, Akasema; "Nikafiri na kila atakaemuunga mkono pia ni kafiri. [29]

Na katika tafsiri ya Al-Qummiy katika kauli yake Allaah

[28] *Furuw'ul-Kaafiy* cha Al-Kulayniyiy uk. 115.
[29] *Bihaarul-Anwaar* cha Al-Majlisiy 69/137-138.

"Na (Allaah) Anakataza uchafu, na uovu, na dhulma, na kila kisichopendeza, hali kadhalika Anakataza kumfanyia ubaya mtu." [An-Nahl 16 : 90].

Wametafsiri (*Al-Fahshaa*-uchafu) kuwa ni Abu Bakr na (*Al-Munkar*-uovu) kuwa ni ´Umar na (*Al-Bagh-yi*-dhulma) kuwa ni ´Uthmaan. [30]

Na ametaja Al-Majlisiy katika *'Bihaarul-Anwaar'* kuwa: "Habari zinazoonesha (elezea) ukafiri wa Abu Bakr na ´Umar na mfano wao, na juu ya malipo ya kuwalaani na kujitenga nao, na habari zinazoelezea uzushi wao ni nyingi kiasi kwamba haitoshi kuelezea katika kitabu hiki au katika vitabu mbalimbali, lakini haya machache tuliyoyataja yanatosha kwa mtu ambae Allaah Kataka kumuongoza katika njia iliyonyooka." [31]

Bali kataja Al-Majlisiy katika *'Bihaarul-Anwaar'* Riwaya mbalimbali kwamba Abu Bakr na ´Umar na ´Uthmaan na Muaawiyah (Radhiya Allaahu ´anhum) kwamba watakuwa katika masanduku ya moto. [32]

Na wanasema (Raafidhwah) katika kitabu chao *'Ihqaaqul-Haq'* cha Al-Mar'ashiy: "Ee Allaah mrehemu Muhammad pamoja na ahli zake, na walaani masanamu wawili wa ki-Quraysh, na Matwaaghuti wao, na mabinti wao..."[33]; Wakiwa wanawakusudia Abu Bakr na ´Umar na Mama wa Waumini ´Aaishah na Hafswah bint ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhum).

Na ametaja Al-Majlisiy katika risala yake aliyoiita "*Al-´Aqaaid*" akasema: Na katika mambo yanayozingatiwa kuwa ni muhimu sana katika dini ya Imaamiyyah ni kuhalalisha Mut´ah, na Hajj tamatui, na kujitenga mbali na; Abu Bakr na ´Umar na ´Uthmaan na Muaawiyah na Yaziyd bin Mu'aawiyah, na kila aliyempiga vita Amiyrul-Muuminiyn ´Aliy). [34]

Na katika siku ya 'Aashuraa (Raafidhwah) huleta mbwa na wakamuita ´Umar, kisha wanaanza kumpiga kwa fimbo na mawe mpaka anakufa, kisha wanaleta mtoto wa Mbuzi kisha wanamuita ´Aaishah na kisha wanaanza kumnyonyoa manyoya yake na kumpiga hadi anakufa. [35]

---

30 Tafsiri ya Al-Qummiy uk. 1/390.
31 *Bihaarul-Anwaar* cha Al-Majlisiy 30/230.
32 *Bihaarul-Anwaar* cha Al-Majlisiy 30/236.
33 *Ihqaaqul-Haq* 1/337. Angalia du´aa ya masanamu wawili mwisho wa kitabu.
34 *Risaalatul-´Aqaaidiy* cha Al-Majlisiy uk. 85.
35 *Tabdiyl-Dhwalaam wa Tanbiyhin-Niyaam* cha Shaykh Ibraahiym Al-Jabhaan uk. 27.

Pia huwa wanasherehekea siku aliyouawa ´Umar bin Al-Khatwaab, na wanamuita Abu Luu-luatil-Majuusiy ambaye alimuua ´Umar kuwa ni shujaa wa dini.[36]

Tunamuomba Allaah Awarehemu Maswahaba wote pamoja wake zake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambao ni Mama wa Waumini.

Hebu tazama ndugu msomaji ubaya na chuki zilizobebwa na kundi hili potofu lililotoka katika Uislamu, na mambo wanayosema juu ya watu wema kama hawa, ambao ndio watu bora baada ya Mitume, watu ambao Allaah Kawasifu, na Mtume wake pia, na Ummah wa Kiislamu umekubaliana juu ya uadilifu wao na ubora wao, bali hata historia inashuhudia ubora wao na juhudi zao kubwa katika Dini hii ya Uislamu.

## Raafidhwah Wanafanana Na Mayahudi

Amesema Shaykhul-Islaam bin Taymiyyah (Allaah Amrehemu):

"Ushahidi juu ya hilo ni kwamba, Matatizo ya Raafidhwah ndio matatizo ya Mayahudi, kwa sababu Mayahudi wanasema: "Ufalme haupaswi kuwa isipokuwa katika kizazi cha Daawuwd, Na Raafidhwah wanadai kuwa utawala (Al-Imaamah) haupaswi kuwa isipokuwa kwa mtoto wa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhu)."

Pia Mayahudi wanasema: "Hakuna Jihaad katika njia ya Allaah mpaka atakapokuja Masiyhud-Dajjaal ashuke na upanga. Na Raafidhwah wanasema: Hakuna Jihaad katika njia ya Allaah mpaka atakapokuja Mahdi na utoke wito wa Jihaad kutoka mbinguni."

Pia Mayahudi huchelewesha Swalah zao mpaka nyota zinapokusanyika,

36 'Abbaasul-Qummiy *'Al-Kunaa wal-Alqaab'* 2/5.

vilevile Raafidhwah nao huchelewesha Magharibi mpaka nyota zikusanyike, ilhali Hadiyth ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) inatufundisha Kwamba: "Hautaacha kuwa ummah wangu katika kheri muda wa kuwa hawaicheleweshi Swalah ya Magharibi mpaka kukusanyika kwa nyota."[37]

Mayahudi waliigeuza Taurat; vilevile Raafidhwah nao wameigeuza Qur-aan. Mayahudi wanapinga jambo la kupangusa katika khufu (soksi); vilevile Raafidhwah wanalipinga jambo hilo. Mayahudi wanamchukia Malaika Jibriyl, wanasema: "Huyo ni adui yetu miongoni mwa Malaika; vilevile Raafidwah wanasema: Jibriyl alikosea kuleta utume kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)."[38]

Vilevile Mayahudi na Wakristo wamewashinda Raafidhwah kwa mambo mawili, kwanza: Waliulizwa Mayahudi: "Ni nani aliye bora katika watu wa mila yenu? Wakasema: "Wabora kwetu ni wafuasi wa Muwsaa.

Na Wakristo wakaulizwa: "Ni nani aliye bora katika mila yenu? Wakasema: Ni wanafunzi wa Nabii ´Iysaa.

Raafidwah wakaulizwa ni nani wabaya zaidi na waovu katika mila yenu?

Wakasema wafuasi wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)[39]

Na ametaja Shaykh ´Abdullaah al-Jamiyliy katika kitabu chake *'Badhlul-Majhuud fiy Mushabahaati Ar-Rafidhwah lil-Yahuwd'* Kwamba katika mambo ambayo Raafidhwah wamefanana na Mayahudi ni, Mayahudi na Maraafidhwah wanawakufurisha watu wote wasiokuwa miongoni mwao na kuzihalalisha damu zao na mali zao, kisha Shaykh akasema: "Mayahudi wanawagawa watu katika mafungu mawili tu (Mayahudi na Ummamiyuwn) Ummamiyuwn ni kila asiyekuwa Yahudi, na wanaitakidi kwamba wao ndio waumini peke yao, Ama Ummamiyuwn wao ni makafiri."

---

[37] Ahmad 4/147, 5/417, 422, Abu Daawuwd 418, Ibn Maajah 689, na katika Az-Zawaaid: Isnaad yake ni Hasan.

[38] Kuna kundi lao liitwalo Al-Ghuraabiyyah linalodai hivyo na hali Jibriyl kasifiwa na Allaah na kapewa sifa ya uaminifu katika Surah mbalimbali; Ash-Shu'araa: 193, At-Takwiyr: 21. Hizi ndizo itikadi wanazoamini Raafidhwah enyi Waislamu tazameni!!

[39] *Minhaajus-Sunnah* cha Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah 1/24.

## Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Juu Ya Maimamu?

Raafidhwah wanadai Maimamu wao ni (Ma'aswuumiyn) - yaani wamehifadhiwa na madhambi, na kwamba wanajua ghayb. Kayanukuu haya Al-Kulayniy katika kitabu *'Uswuwlul-Kaafiy'*: "Kasema Imamu Ja'afar Asw-Swaadiq: Sisi ni hazina ya elimu ya Allaah, sisi ni wafasiri wa amri za Allaah, Sisi ni watu tuliokingwa na dhambi, imeamrishwa tutiiwe, na imekatazwa tusiasiwe, Sisi ndio hoja ya Allaah ya wazi kwa viumbe vilivyo chini ya ardhi na mbingu na vilivyo juu ya Ardhi."[40]

Pia kasema Al-Kulayniy katika *'Al-Kaafiy'* Katika mlango aliouita mlango kuhusu (kwamba Maimamu pindi wanapotaka kujua jambo basi hujua tu). Imepokewa toka kwa Ja'afar kwamba amesema: "Hakika Imamu anapotaka kujua basi hujua tu, na kwamba wao wanajua muda wa kufa kuwa ni lini, na kwamba wao hawafi ila kwa hiyari yao wenyewe."[41]

Na amesema Al-Khumayniy (Khomeini) katika kitabu chake *'Tahriyrul-Wasiylah'* kwamba "Hakika Imamu anayo nafasi tukufu, na daraja ya juu, na utawala wa kufanya kila kitu viko chini ya utawala wake vyote vilivyo katika ulimwengu" na akasema pia "Hakika sisi (anakusudia Maimamu wa Ithnaa-´Ashariyyah) tunazo hali fulani kwa Allaah ambazo hazipati Malaika wala Nabii yoyote."[42]

Imekuja katika kitabu cha Mayahudi *'At-Tilmuud'* Kwamba: "Mataifa yote wasiokuwa Mayahudi ni Washirikina."

Wamemkufurisha hata Nabii ´Iysaa (´Alayhis-Salaam), kama ilivyokuja katika *At-Tilmuud*, wamemsifu na kumtaja kuwa ni kafiri, wala hamjui Allaah. Raafidhwah nao wanaitakidi kwamba wao ndio waumini peke yao, na kila ambae si Raafidhwah basi ni kafiri wala hana fungu lolote katika Uislamu.

Ama kuhusu sababu za Raafidhwah kuwakufurisha Waislamu ni kwa kuwa hawaitakidi '*Al-Wilaayah*' Ambayo ndio itikadi ya Raafidhwah, na kwamba jambo hili ni nguzo katika nguzo za Uislamu na kila asiyeitakidi hivi basi huyo ni kafiri kwa mujibu wa imani yao ni kama ambae hajatamka shahaadah mbili, au ni sawa na aliyeacha Swalah tano, bali *'Al-Wilaayah'* kwao ni jambo ambalo limetangulizwa juu ya nguzo zote za Uislamu.

---

40 *Uswuwl-ul-Kaafiy* cha Al-Kulayniyiy 1/165.

41 *Uswuwl-ul-Kaafiy* cha Al-Kulayniyiy 1/258.

42 *Tahriyrul-Wasiylah* cha Al-Khumayniy (Khomeini) uk. 52,94.

Amepokea Al-Barqiyu kutoka kwa Abu ´Abdullaah (´Alayhis-Salaam) kwamba amesema: "Hakuna yeyote anayefuata mila ya Ibraahiym isipokuwa sisi tu na wafuasi wetu, ama watu wengine wote wamejitenga na mila yake."

Na imekuja katika tafsiri ya Al-Qummiy, kuwa imepokewa kutoka kwa Abu ´Abdillaah (´Alayhis-Salaam) kwamba amesema: "Hakuna yeyote aliye katika mila ya Uislamu isipokuwa sisi, mpaka siku ya Qiyaamah."[43]

Bali imefikia hali kwa Maraafidhwah waliochupa mipaka katika kuwatukuza na kuwafadhilisha (kuwafanya bora) Maimamu wao, wamewafanya bora juu ya Manabii wote isipokuwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).[(44)]

Hawakuishia hapo tu, bali wanasema kuwa Maimamu wao wana utawala wa mwisho kabisa. Ameyataja haya Al-Khui katika kitabu chake *'Miswbaahul-Faqaaha'* akasema: Ni wazi kwamba hakuna shaka kabisa juu ya utawala wao juu ya viumbe wote, kama ilivyobainisha katika maneno yao, kwa kuwa wao ndio sababu ya ulimwengu, na wao ndio sababu ya kupatikana viumbe, maana kama si wao basi watu wote wasingeliumbwa, bali wameumbwa kwa ajili yao, na kuwepo kwao ni kwa ajili yao… na utawala walionao Maimamu ni kama utawala wa Allaah juu ya viumbe wake."[(45)]

Tunamuomba Allaah Atulinde na upotofu wao huu!

Vipi Maimamu wawe ndio sababu ya kupatikana viumbe? Vipi wawe sababu ya kuwepo ulimwengu? Vipi watu wote waumbwe kwa ajili ya Maimamu wao, ilhali Allaah Anasema: katika Surat Adh-Dhaariyaat: 56,

"Sikuwaumba majini na watu ila tu wapate kuniabudu."

Tunamuomba Allaah Atukinge na itikadi potofu kama hii inayopingana na Qur-aan na Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Kasema Shaykhul-Islaam ibn Tayimiyyah (Wanadai Raafidhwah kuwadini inafuata matakwa ya Wanavyuoni wao, halali ni ile wanayoihalalisha wao, na haramu ni ile wanayoiharamisha wao, na dini ni yale wanayoyataka wao."[(46)]

---

43 *Badhlul-Majhuwd fiy Mushaabahat Ar-Raafidhwah Lil-Yaahuwd* cha Shaykh ´Abdullaah al-Jamiyliy 2/559, 568. Kwa ziada kuhusu namna Mashia wanavyowakufurisha Waislamu, rejea kitabu *'Ash-Shiy'at Al-Ithnaa-'Aashariyyah wat-Takfiyruhum Li-'Umuwmil-Muslimiyn'.*

44 *Mir-aatul-´Uquwl fii sharhi Akhbaarir Rasuwl* cha Al-Majlisiy 2/290.
45 *Miswbaahul-Fuqaaha* cha Abul-Qaasim Al-Khuiy 5/33.
46 *Minhaajus-Sunnah cha Shaykhul-Islaam* Ibn Tayymiyyah 1/482.

## Ni Ipi Itikadi Ya Kurejea Wanayoiamini Raafidhwah?

Raafidhwah wamezua Bid´ah (uzushi) wanaouita *'Ar-Raj'ah'*, kasema Al-Mufiyd kuwa: "Wamekubaliana Imaamiyyah juu ya kurudi (kufufuka) wengi katika watu waliokufa."[47]

Na itikadi hii inakusudia kufufuka kwa Imamu wao wa mwisho wanayemuita 'Al-Qaaim' atatoka katika zama za mwisho akitokea katika pango, ambaye atakuja kuwaua wapinzani wake wote na kuwarejeshea Mashia haki zao walizoporwa na makundi mbalimbali katika historia ya kuwepo kwao. [48]

Amesema As-Sayyid Al-Murtadhwaa katika kitabu chake *'Al-Masaailu An-Naaswiyriyyah'* kwamba Abu Bakr na ´Umar, watasulubiwa katika zama hizo (za kutoka kwake) huyo Imamu wao wa kumi na mbili wanayemuita *'Qaaimu Aali Muhammad'* na kwamba mti utakuwa mbichi kabla ya kusulubiwa kwao lakini baada ya kusulubiwa kwao utakauka. [49]

Na amesema Al-Majlisiy katika kitabu *'Haqul-Yaqiyn'* kutoka kwa Muhammad Al-Baaqir: "Pindi atakapodhihiri Al-Mahdi, basi atamfufua bibi ´Aaishah kisha amsimamishie *hadd* (adhabu)."[50]

Kisha wakayapanua makusudio na maana ya *Ar-Raj'ah* na kudai kuwa Mashia wote watafufuka na Maimamu wao, na wagomvi wao nao watafufuka na Maimamu wao. Itikadi hii potofu inatubainishia chuki kubwa zilizofichika katika nafsi zao ambazo zinawapelekea kueleza upotofu kama huu, na itikadi hii ndio iliwapelekea As-Sabaaiyyah wakakanusha kuwepo siku ya mwisho.

Na madhumuni ya kurejea ni kulipiza kisasi kwa wagomvi wao, lakini ni akina nani wagomvi wao? Riwaya ifuatayo itakubainishia ndugu msomaji chuki waliyonayo Raafidhwah dhidi ya Ahlus-Sunnah, na jinsi walivyo karibu zaidi na Mayahudi na Manaswara. Ameeleza Al-Majlisiy katika kitabu chake *'Bihaarul-Anwaar'*, kutoka kwa Abu Baswiyr kapokea toka kwa Abu ´Abdillaah amesema: Alisema: "Ewe Abu Muhammad: Kana kwamba ninatazama kushuka kwa Al-Qaaim katika Masjidus-Sahlah akiwa na watu wake na familia yake…. mpaka akasema… nikamwambia, atakuwa na msimamo gani kuhusu Ahludh-Dhimmah?

---

47 *Awaail-ul-Maqaalaat* cha Al-Mufiyd uk. 5.
48 *Al-Khtuwtwul-'Ariydhwah* cha Muhibbud-Diyn Al-Khaatwiyb uk. 80.
49 *Awaailul-Maqaalaat* cha Al-Mufiyd uk. 95.
50 *Haqul-Yaqiyn* cha Muhammad Al-Baaqir Al-Majlisiy uk. 347.

Akasema: “Atawapa amani kama alivyowapa amani Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), na watatoa kodi hali ya kuwa ni madhalili, nikasema, je, waliokufanyieni uadui? Akasema: “Hapana ewe Abu Muhammad, yeyote aliyetukhalifu katika dola yetu hatokuwa na nafasi yoyote, hakika Allaah Katuhalalishia damu zao, wakati atakapokuja Al-Qaaim, na pindi atakaposimama huyo msimamaji wetu, atalipiza kisasi kwa ajili ya Allaah na Mtume Wake na kwa ajili yetu pia.”[51]

Hebu tazama ndugu Muislamu jinsi gani huyo Mahdi wa Mashia atawapa amani Mayahudi na Manaswara, halafu awapige vita Ahlus-Sunnah!

## Ni Ipi Itikadi Ya "Taqiyyah" Kwa Raafidhwah?

Amesema mmoja wa Wanavyuoni wao wa zama hizi kuwa:

"Taqiyyah ni kitendo cha mtu kusema au kufanya kinyume na vile anavyoitakidi, kwa lengo la kujikinga na madhara yeye au mali yake au kulinda utu na heshima yake."[52]

Na wanadai kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alifanya Taqiyyah wakati alipokufa kiongozi wa wanafiki ´Abdullaah bin Ubay bin Saluwl, pindi alipokuja kumswalia, kisha ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhu) akamwambia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). “Hivi Allaah si kakukataza kumswalia mtu huyu mnafiki?, Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamwambia wewe unajua ni nini nimesema? Nimesema: “Ee Mola wangu mjaze ndani yake moto, na ulijaze kaburi lake moto, na umuingize motoni."[53]

Hebu tazama ndugu yangu Muislamu vipi wanamzulia na kumnasibisha Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na uongo?!

Hivi inaingia akilini kwamba Maswahaba wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wanamtakia Rahma na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akimlaani?!

---

51 *Bihaarul-Anwaar* cha Al-Majlisiy 25/376.

52 *Ash-Shi’at fiyl Miyzaan*, cha Muhammad Jawaad Mughniyah uk. 47.

53 *Furuw’ul-Kaafiy*, *Kitaabul Janaaiz* uk. 188.


www.alhidaaya.com

Na amenukuu Al-Kulayniy katika *'Uswuwlul-Kaafiy'*: "Kasema Abu ´Abdillaah: "Ewe Abu ´Umar hakika asilimia tisa ya dini ipo katika taqiyyah, na hana dini asiyekuwa na Taqiyyah, na Taqiyyah inaingia katika kila kitu isipokuwa katika pombe na kupangusa juu ya khufu."

Na amenukuu vilevile Al-Kulayniy toka kwa Abu ´Abdillaah kwamba amesema: "Icheni dini yenu, na ikingeni kwa Taqiyyah, kwa hakika hana imani asiyekuwa na Taqiyyah."[54]

Bali imefikia hali kwa Raafidhwah wanajuzisha kuapa kwa asiyekuwa Allaah kwa mujibu wa Taqiyyah!!

Ameyaeleza hayo Al-Huru Al-'Aamiliy katika kitabu chake *'Wasaailu Ash-Shi'ah'* kuwa imepokewa kutoka kwa Abu Bukayr, kutoka kwa Zuraarah kutoka kwa Abu Ja'afar (Radhiya Allaahu ´anhu) amesema: "Nilisema kumwambia Abu Ja'afar: "Hakika sisi tunapita kwa watu wanatutaka tuape juu ya mali zetu na ilihali tumeshakwishazitolea Zakaah, akasema (Abu Ja'afar): Ewe Zuraarah pindi utakapochelea hilo basi wewe apa kwa vyovyote vile watakavyotaka, nikamuuliza: Hata kuapa kwa talaka? Akasema kwa chochote watakachotaka."

Na imepokewa toka kwa Suma'ah toka kwa Abu ´Abdillaah amesema:

"Pindi mtu atakapoapa kwa Taqiyyah hakuna tatizo maadam kalazimishwa, na kalazimika kufanya hivyo."[55]

Raafidhwah wanaitakidi kuwa Taqiyyah ni faradhi ambayo madhehebu yao hayasimami bila ya Taqiyyah, na wanaitumia hasa hasa katika mazingira magumu, hivyo inatakiwa ndugu Muislamu utahadhari sana na hawa Raafidhwah.

54 *Uswuwlul-Kaafiy* cha Al-Kulayniy uk. 482-483.
55 *Wasaail Ash-Shi'ah* cha Al-Hurru Al-'Aamiliy 16/136-137.

## Ni Ipi Itikadi Ya Udongo Wanayoiamini Raafidhwah?

Makusudio ya udongo katika itikadi ya Raafidhwah, ni udongo wa kaburi ya Husayn (Radhiya Allaahu ´anhu) ameeleza mmoja wa wapotevu miongoni mwao aitwae Muhammad An-Nu'umaan Al-Haarithiy, ambae wanamuita *'Ash-Shaykh Al-Mufiyd'* katika kitabu chake *'Al-Mazaar'* imepokewa kutoka kwa Abu ´Abdillaah kwamba amesema: "Katika udongo wa kaburi ya Husayn, kunapatikana ponyo la kila maradhi, nao ndio dawa iliyo kubwa kabisa."

Na amesema ´Abdullaah: "Wafanyieni tahniki (yaani watilieni mdomoni mara tu baada ya kuzaliwa kwao) watoto wenu kwa udongo wa kaburi la Husayn."

Na akasema vilevile: "Alitumiwa ´Abdul-Husayn Ar-Ridhwaa mzigo (furushi la nguo) kutoka Khurasaan ndani yake mkiwa na udongo, akaulizwa alietumwa mzigo huo, ni kitu gani hiki? Akasema: "Huu ni udongo kutoka katika kaburi la Husayn."

Hapakuwa panatumwa mzigo wowote isipokuwa ndani yake panawekwa udongo, anasema: Udongo huu ni amani kwa idhini ya Allaah.

Na inasemakana kwamba mtu mmoja alimuuliza Asw-Swaadiq (Abu 'Abdillaah) kuhusu kutumia udongo wa kaburi la Husayn, akajibu kumwambia: Pindi utakapoula basi sema hivi: "Ewe Mola wangu hakika mimi nakuomba kwa haki ya ufalme ulioushika, na kwa haki ya Mtume aliyehifahiwa, nakuomba umpe Rahma Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pamoja na watu wa nyumba yake, na Ujaalie udongo huu kuwa ni ponyo la kila ugonjwa, na uwe ni kitulizo cha amani kutokana na kila khofu, na ni ulinzi kutokana na kila baya."

Pia Raafidhwah wanadai kwamba, Mashia wameumbwa kwa udongo maalum, na Sunni wameumbwa kwa udongo mwengine kisha ukachanganywa udongo huo wote, basi maasi na maovu yanayofanya Mshia yeyote ni kutokana na athari ya udongo walioumbiwa Masunni. Na kheri na uongofu anaekuwanayo Sunni yeyote ni kutokana na athari za Udongo walioumbwa Shia. Pindi itakapofika siku ya Qiyaamah, basi maovu ya Mashia watabebeshwa Masunni, na mema ya Masunni watapewa Shia. (56)

56 *'Ilalu Ash-Sharaai'* uk. 490-491. *Bihaarul-Anwaar* 5/247-248.

### Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Ahlus-Sunnah?

Miongoni mwa itikadi mbaya za Raafidhwah ni kwamba wanahalalisha damu na mali za Ahlus-Sunnah amepokea Asw-Swaadiq katika *'Al-'Ilal'* kutoka kwa Daawuwd bin Farqad amesema: "Nilimuuliza Abu ´Abdillaah, unasemaje kuhusu Naaswibiy? (Naswibi wanakusudia Ahlus-Sunnah), akasema: Damu yake ni halali, hata kama utaweza kumuangushia ukuta au kumzamisha baharini basi fanya hivyo. Nikamuuliza vipi kuhusu mali yake? Akasema pindi utakapoweza kuichukua basi ichukue."[57]

Pia Raafidhwah wanaitakidi kwamba kizazi chao ndio kizazi safi.

Ameeleza Haashim Al-Bahraaniy katika tafsiri yake *'Al-Burhaan'* imepokewa toka kwa Maytham bin Yahya, kutoka kwa Jaabir bin Muhammad, amesema: "Hakuna mtoto yeyote azaliwaye isipokuwa Ibliys anakuwa haadhwir katika kuzaliwa kwake, anapojua mtoto huyo ni katika Shia basi shaytwaan mkubwa anamkinga huyo mtoto kutokana na Ibliys, na kama si katika Shia basi shaytwaan huingiza kidole chake katika sehemu zake za nyuma (katika makalio ya mtoto), na hii ndio sababu ya kuwa mtoto wa kiume huzaliwa kaelekea chini, na kama ni mtoto wa kike basi shaytwaan huingiza kidole chake katika utupu wake, hivyo anazaliwa akiwa ni muovu, na ndio maana mtoto huzaliwa analia sana."[58]

Bali Mashia wanaitakidi kwamba watu wote ni watoto wa zina isipokuwa Shia peke yao!!

Ameeleza Al-Kulayniy katika kitabu chake *'Ar-Rawdhwatu Minal-Kaafiy'* kutoka kwa Abu Hamzah, kutoka kwa Abu Ja'afar kwamba amesema: "Nilisema kumwambia, hakika baadhi ya jamaa zetu wanazua uongo na kuwatuhumu wasio waungu mkono, akamjibu kuwa, kuachana nao ni bora zaidi, kisha akasema: "Wa-Allaahi ewe Abu Hamzah hakika watu wote ni watoto wa zinaa isipokuwa Shia."[59]

Na katika itikadi za Raafidhwah wanaona kwamba Ahlus-Sunnah ukafiri wao ni mkubwa zaidi kuliko ukafiri wa Mayahudi na Manaswara, kwa sababu wao

---

57 *Al-Mahaasin An-Nafsaaniyah* uk. 166.
58 *Tafsiyrul-Burhaaniy* cha Haashim Al-Bahraaniy 2/300.
59 *Ar-Rawdhwatul Minal-Kaafiy* cha Al-Kulayniyiy 8/285.

asili yao ni Makafiri, kwa wao Mashia, Ahlus-Sunnah wameritadi, na ukafiri wa kuritadi ni mkubwa zaidi, hii ni kwa mujibu wa ijmai'.

Ndio maana (Mashia) wanakuwa bega kwa bega dhidi ya Waislamu, kama historia inavyojieleza.[60]

Imekuja katika kitabu *'Wasaailu Ash-Shi'ah'* kutoka kwa Al-Fudhwayl bin Yasaar amesema: "Nilimuuliza Abu Ja'afar, je naruhusiwa kumuozesha Naaswibiy (wakimaanisha Sunni) mwanamke wa ki-Raafidhwah? Akasema: Hapana, kwa sababu Naaswibiy ni kafiri."[61]

Na Manaswibi kwa Ahlus-Sunnah ni wale ambao wanamchukia ´Aliy bin Abi Twaalib (Radhiya Allaahu ´anhu), lakini Raafidhwah wao wanawaita Ahlus-Sunnah Naaswibiy, kwa sababu wanamtanguliza Abu Bakr na ´Umar na ´Uthmaan juu ya ´Aliy, pamoja na kwamba kumtanguliza Abu Bakr na ´Umar na ´Uthmaan juu ya ´Aliy ndivyo ilivyokuwa zama za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), na ushahidi wa haya ni kauli ya Ibn ´Umar:

"Tulikuwa tukifadhilisha baina ya watu katika zama za (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), hivyo basi, tulikuwa tunamfadhilisha Abu Bakr kisha ´Umar kisha ´Uthmaan." [Al-Bukhaariy].

Na amezidisha At-Twabraaniy katika '*Al-Kabiyr*':

"Na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), alikuwa akilijua hilo wala hatukemei katika hilo."

Pia Ibn Asaakir amepokea:

---

[60] Anasema Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah (Allaah Amrehemu) kuwa Raafidhwah (Mashia) walikuwa wakisaidiana na Tatar walipovamia nchi za Waislamu. Al-Fataawaa 35/151. Tazama na kitabu *'Kayfa Dakhala Tatar fiy Bilaadil-Muslimiyn'* cha Dr. Sulaymaan Hamad. Na kumbuka ndugu Muislamu namna Shia walivyoshirikiana na wavamizi (Marekani na wenzake) huko Iraq karibuni na kufanya mauaji ya kinyama ya watu wengi wasio na hatia hususan katika mji wa Faluja na miji mingine ya Iraq!!

[61] *Wasaail Ash-Shi'ah* cha Al-Hurru Al-'Aamiliy 7/431, na *At-Tahdhiyb* 7/303.

"Tulikuwa tukimfadhilisha Abu Bakr na ´Umar na ´Uthmaan na ´Aliy".

Amepokea Imaam Ahmad na wengineo kutoka kwa ´Aliy bin Abi Twaalib kwamba amesema:

"Mbora wa Ummah huu baada ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Abu Bakr kisha ´Umar, na laiti ningependa ningemtaja wa tatu." Amesema ImaamuAhmad kwamba athar hii ni Mutawaatir.[62]

## Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Ndoa Ya Mut'ah Na Ina Ubora Gani Kwao?

Ndoa ya Mut'ah ina fadhila kubwa kwa Raafidhwah, kama wanavyodai. Imekuja katika kitabu *'Manhajus-Swaadiqiyn'* cha Fat-hullaah Al-Kaashaan, kapokea toka kwa Asw-Swaadiq: "Hakika Mut'ah ni katika dini yangu na dini ya baba yangu, basi mwenye kuifanya hiyo anatekeleza dini yetu, na mwenye kuipinga, huyo atakuwa anaipinga dini yetu, bali huyo anaifuata dini nyingine isiyokuwa dini yetu, na mtoto anaezaliwa katika ndoa ya mut'ah ni bora kuliko anayezaliwa katika ndoa ya kawaida, na mwenye kuipinga mut'ah huyo ni kafiri ameritadi."[63]

Amenukuu Al-Qummiy katika kitabu *'Man Laa Yahdhwuruhul-Faqiyh'* kutoka kwa ´Abdullaah bin Sinaaniy, kutoka kwa ´Abdullaah amesema: "Hakika Allaah Mtukufu Katuharamishia kinywaji chochote chenye kulevya, na akatupa badala yake mut'ah."[64]

Na imekuja katika *'Tafsiyr Manhajis-Swaadiqiyn'* ya Mullaa Fat-hullaah Al-Kaashaaniy: "Amesema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), mwenye kufanya mut'ah mara moja, basi huachwa huru na moto theluthi yake, na mwenye kufanya mara mbili huachwa huru na moto theluthi mbili, na mwenye kufanya mara tatu, basi huachwa huru na moto yeye mzima."

---

62 *At-Taaliqaat ´alaa Matni Lumu´atil-I´itiqaad* cha Shaykh Jibriyn uk. 910.

63 *Tafsiyr Manhajis-Swaadiqiyn* cha Mullaa Fut-hullaah Al-Kaashaaniy 2/495.

64 *Man Laa yahdhwuruhul-Faqiyh* cha Ibn Baabawayhi Al-Qummiy uk. 330.

Na katika kitabu hicho hicho, imekuja kuwa "Kasema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), mwenye kufanya mut'ah mara moja, basi huyo kasalimika na ghadhabu za Allaah, na atakayefanya mara mbili atafufuliwa pamoja na watu wema, na atakayefanya mara tatu huyo atakuwa nami peponi."

Pia katika kitabu hicho hicho kwamba amesema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), mwenye kufanya mut'ah mara moja, anakuwa katika daraja ya Husayn, na mwenye kufanya mut'ah mara mbili yuko katika daraja ya Hassayn, na mwenye kufanya mut'ah mara tatu, anakuwa katika daraja ya ´Aliy bin Abi Twaalib, na mwenye kufanya mara nne daraja yake ni kama daraja yangu,"(65)

Na Marafidhwah hawakuainisha idadi maalumu katika suala la mut'ah, imekuja katika *'Furuw'ul-Kaafiy'* na *'At-Tahdhiyb'* na *'Al-Istibswaar'* kutoka kwa Zuraarah kapokeya toka kwa Abu ´Abdillaah, kasema: "Aliulizwa kuhusu mut'ah kwamba je ni katika wanawake wanne walioruhusiwa? Akasema: Waweza kuoa mpaka elfu moja, kwa sababu wao ni wenye kukodiwa.

Na pia imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Muslim, kutoka kwa Abu Ja'afar kwamba, alisema kuhusu ndoa ya mut'ah: Kwamba hao si katika wale wanne, kwa sababu mwanamke anayeolewa ndoa ya mut'ah hapewi talaka, wala hana fungu lolote katika mirathi, bali yeye ni mwenye kukodiwa tu."(66)

Vipi hali hii na ilihali Allaah Anasema:

"Na wale ambao tupu zao wanazilinda. Isipokua kwa wake zao au kwa (wanawake) wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, basi hao ndio wasiolaumiwa. (Lakini) anayetaka kinyume cha haya basi hao ndio warukao mipaka (ya Allaah)." [Al-Mu-uminuwn: 5-7].

Kwa hiyo Aayah hizi zinatubainishia kwamba ndoa zinazoruhusiwa ni mke na wale iliyowamiliki mikono ya kuume, na kinyume na hawa basi ni haramu, hivyo mut'ah ni zinaa, tunamuomba Allaah Atukinge na shari.

Amesema Shaykh ´Abdullaah bin Jibriyn kwamba: "Raafidhwah katika kuhalalisha mut'ah wanaitumia Aayah iliyokuja katika Suratun Nisaa Aayah ya 24:

"Na pia (mmeharamishiwa) wanawake wenye (waume zao) isipokua wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume (ndio) shari'ah ya Allaah juu yenu. Na

65 *Tafsiyr Manhajis-Swaadiqiyn* cha Mullaa Fut'hullaah Al-Kaashaniy 2/492-493
66 Al-Furuu minal-Kaafiy cha Al-Kulayniyiy 5/451 na At-Tahdhib 2/188.

mmehalalishiwa (kuoa wanawake) wasio hawa muwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila ya kufanya zinaa. Basi wale mnaowaoa miongoni mwao wapeni mahari yao yaliyolazimishwa. Wala si vibaya kwenu katika (kutoa) yale mliyoridhiana badala ya yale yaliyotajwa. Hakika Allaah ni mjuzi na mwenye hekima." [An-Nisaa: 24].

Na jawabu la hoja hii ni kwamba: Hakika Aayah zote hizi kuanzia aayah ya 19 hadi aayah ya 23 zinazungumzia ndoa,

"Enyi mlioamini! Si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu." [An-Nisaa: 19].

"Na mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke…" [An-Nisaa: 20].
Hadi kauli Yake:

"Wala msiwaoe wake waliowaoa baba zenu..." [An-Nisaa: 22].
Hadi kauli Yake:

"Mmeharimishiwa mama zenu..." [An-Nisaa: 23].

kisha baada ya kutaja wale walioharamishwa kwa nasabu na kwa sababu zingine Akasema Allaah:

"Mmehalalishiwa wanawake wengine wasiokuwa hawa waliotajwa..." [An-Nisaa: 24].

Maana yake, imehalalishwa ndoa kwa wanawake wote waliobaki, hivyo, mkiwaoa kwa ajili ya kustarehe nao (kuwaingilia), basi muwape mahari yao ambayo mmefaradhishiwa kwao.

Hivyo ndivyo walivyoifasiri Aayah hii kongamano la Maswahaba na waliokuja baada yao."(67)

---

67 Ni katika maneno ya Shaykh Ibn Jibriyn na dalili nyingine ya kuharamisha mut`ah katika Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Hadiyth ya Rabiy'u bin Saburah Al-Juhaniy kwamba baba yake alimuhadithia kwamba alikuwa pamoja na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Enyi watu hakika mimi nilikuwa nimekuruhusuni kufanya Mut`ah, hakika Allaah Ameiharamisha mpaka siku ya Qiyaamah, yeyote atakayekuwa na mwanamke ambaye kamuoa ndoa ya Mut`ah basi na amuache, na wala asichukue chochote alichokuwa kampa." [Muslim 1406].

Hata Sheikh wa kundi lao hilo, Atw-Twuwsiy katika kitabu chake *'Tahdhiybul-Ahkaam'* ameitaja kwa ubaya ndoa ya Mut`ah, anasema: "Kama akiwa mwanamke anatoka katika nyumba ya watu watukufu basi haifai kumuoa katika ndoa ya mut`ah, kwa kuchelea aibu itakayoipata familia yake na udhalili utakaompata yeye."(68)

Bali hali imefikia kwa hawa Raafidhwah wanahalalisha kumuendea mwanamke kinyume cha maumbile (nyuma). Yamekuja haya katika *'Al-Istibswaar'* kutoka kwa ´Aliy bin Al-Hakam amesema: "Nilimsikia Swafwaan anasema: Nilimuuliza Ar-Ridhwaa nikasema: Hakika mmoja katika wafuasi wako kanituma nikuulize jambo ambalo yeye kaogopa na kaona aibu kukuuliza, akasema: Ni lipi? Akasema: Je, inafaa mtu kumuingilia mke wake kinyume cha maumbile (nyuma)? Akasema: "Ndio inafaa."(69)

## Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Najaf Na Karbalaa, Na Je, Kuna Fadhila Gani Katika Kuzuru Sehemu Hizi?

Mashia wanaitakidi sehemu yalipo makaburi ya watu waliodai kuwa ni Maimamu wao, au ambao ni Maimamu kweli, kwa sehemu hizo ni sehemu takatifu, hivyo Al-Kuufa ni *haram* (sehemu takatifu), pia Karbalaa ni *haram*, na Qumm nayo ni *haram*. Na wanayo riwaya wanayodai kuwa imepokelewa kwa As-Swaadiq kwamba, Allaah Anayo *haram* Yake ambayo ni Makkah, na Mtume Wake anayo *haram* yake ambayo ni Madiynah, na Amiyrul-Muuminiyna (´Aliy) anayo *haram* yake ambayo ni Al-Kuufah, na sisi tunayo *haram* yetu ambayo ni Qumm.

Na Kar-balaa kwa Mashia ni bora kuliko Al-Ka´abah. Imekuja katika Kitabu *'Bihaarul-Anwaar'* kutoka kwa Abu ´Abdillaah kwamba kasema:

"Hakika Allaah Aliiteremshia Al-Ka´abah wahyi (ufunuo) lau kama si udongo wa Karbalaa nisingelikufanya bora, na lau kama si mwili wa yule aliyeko katika udongo wa Karbalaa nisingekuumba, wala nisingeumba nyumba ambayo

68 *Tahdhiybul-Ahkaam* cha Atw-Twuwsiy 7/227.
69 *Al-Istibswaar* cha Atw-Twuwsiy 3/243.

kwayo umejifakharisha, basi tulia na uwe ni Mkia dhalili na si mwenye kibri kwa ardhi ya Karbalaa, la sivyo nitakutupa katika Jahannam."[70]

Bali Raafidhwah wanaona kuzuru kaburi la Husayn huko Karbala ni bora kuliko nguzo ya tano ya Uislamu (Hijjah)!!

Amesema Al-Majlisiy katika kitabu chake *'Bihaarul-Anwaar'* kutoka kwa Bashiyr Ad-Dahaan amesema: "Nilimuuliza Abu ´Abdillaah: "Endapo itanipita Hijjah kisha nikaenda katika kaburi la Husayn? Akasema: Vizuri sana ewe Bashiyr, Muumini yeyote atakaeliendea kaburi la Husayn hali ya kutambua haki yake, katika siku ambayo si siku ya 'Iyd, basi huandikiwa thawabu za Hijjah 20 na ´Umrah 20 zenye kukubaliwa, na thawabu za kushiriki katika vita 20 vya Jihaad pamoja na Mtume au Imamu muadilifu, na atakayeliendea siku ya ´Arafah hali ya kujua haki zake basi huandikiwa thawabu za Hijjah 1000 na ´Umrah 1000 zenye kukubaliwa, na thawabu za kupigana Jihaad 1000 pamoja na Mtume au Imamu muadilifu.

Pia katika kitabu hicho hicho wametaja kwamba wanaozuru kaburi la Husayn huko Karbalaa ni watu safi, na wanaokuwa wamesimama ´Arafah ni watoto wa Zinaa!!

Imepokewa toka kwa ´Aliy bin Asbaatw kwamba kapokea toka kwa Abu ´Abdillaah kuwa kasema: "Hakika Allaah Mtukufu Anaanza kuwatazama wanaozuru kaburi la Husayn usiku wa kuamkia ´Arafah. Akasema: Nikamuuliza, kabla hajawatazama walioko katika kisimamo cha ´Arafah? Akasema: Ndio, nikamuuliza, kwanini iwe hivyo? Akasema: "Kwa sababu katika watu walioko ´Arafah mna watoto wa zinaa tofauti na wale walioko Karbalaa hakuna mtoto wa zinaa kati yao."[71]

Bali kiongozi wao mkuu (wa hivi sasa) ´Aliy As-Sistaaniy katika kitabu chake *'Minhaajus-Swaalihiyn'* amefadhilisha kuswali katika makaburi kuliko kuswali katika Misikiti!!

Kasema katika mas-alah nambari 562: "Inapendeza kuswali katika makaburi ya Maimamu (´Alayhimus-Salaam) bali imesemekana kuwa ni bora kuliko kuswali Misikitini, na imepokewa kwamba kuswali katika kaburi la Imamu ´Aliy bin Abi Twaalib ('Alayhis Salaam) ina ubora wa Swalah laki mbili.˝[72]

Bali Shaykh wao 'Abbaas Al-Kaashaaniy katika kitabu chake *'Maswaabiyhul-Jinaan'* kapituka mipaka katika kuitukuza Karbalaa mpaka akasema: "Hapana

70 Bihaarul-Anwaar 10/107.
71 *Bihaarul-Anwaar* cha Al-Majlisiy 85/98.
72 *Minhaajus-Swalihiyn* cha As-Sistaaniy 1/187.

shaka kwamba Karbalaa ndio sehemu takatifu zaidi katika Uislamu, na imepewa utukufu ambao haikupewa sehemu yoyote ardhini, na hii ni kwa mujibu wa dalili nyingi zilizopokewa kuhusu jambo hili, hivyo ikafanywa ndio ardhi ya Allaah iliyotukuzwa na kubarikiwa, na ni ardhi iliyonyenyekea, na ni ardhi iliyoteuliwa na ndio *haram* ya Allaah yenye baraka na amani, na ndio *haram* ya Mtume, na ndio kitovu cha Uislamu, na ni katika sehemu ambazo Allaah Anapenda kuombwa na kuabudiwa katika sehemu hizo, na ndio ardhi ambayo udongo wake ni tiba, hakika sifa hizi na nyinginezo zilizopo katika ardhi ya Karbalaa, hazipatikani katika sehemu yoyote ardhini, hata katika Al-Ka´abah."[73]

Vilevile imekuja katika kitabu *'Al-Mazaar'* cha Muhammad An-Nu'umaan, wenyewe wanamuita *'Ash-Shaykhul-Mufiyd'* akielezea ubora wa Masjid Al-Kuufah: Imepokewa toka kwa Abu Ja'afar Al-Baaqir amesema: "Lau watu wangejua fadhila zinazopatikana katika Masjid Al-Kuufah basi wangeliuandalia matumizi na vipandwa kutoka sehemu mbalimbali ili kuuendea, hakika Swalah ya faradhi katika Msikiti huo ni sawa na Hijjah, na Swalah ya Sunnah ni sawa na `Umrah."[74]

Vilevile imekuja katika kitabu hicho hicho katika mlango aliyouita 'Yasemwayo wakati wa kusimama katika kaburi' kwamba mwenye kumzuru Husayn anatakiwa kuashiria kwa mkono wake wa kuume, na aseme katika du´aa ndefu kabisa, miongoni mwake maneno yafuatayo: "Nimekujia kukuzuru, nikitaraji uthibitishwe unyayo wangu, na nina yaqini kwamba Allaah Mtukufu Anawaondolea waja Wake matatizo yao kupitia kwenu, na kwa sababu yenu anateremsha Rahma, na kupitia nyinyi anaizuia ardhi isiwadidimize watu wake, na kupitia nyinyi kayathibitisha majabali yake. Ninamuelekea Mola wangu kupitia kwenu ili mnikidhie haja zangu, na mnisamehe madhambi yangu." [75]

Hebu tazama ndugu msomaji jinsi watu hawa walivyotumbukia katika ushirikina, kwa kumuomba asiyekuwa Allaah awakidhie haja zao, na kuomba

73 *Maswaabiyhul-Jinaan* cha ´Abbaas Al-Kaashaaniy uk. 360.
74 *Kitaabul-Mazaar* cha Shaykh Al-Mufiyd uk. 20.
75 *Kitaabul-Mazaar* cha Shaykh Al-Mufiyd uk. 99.

kusamehewa madhambi yao kwa asiyekuwa Allaah, vipi wamefikia katika hali hii, na ilihali Allaah Anasema:

"Hakuna anayesamehe madhambi ila Allaah." [Al-´Imraan 03: 135].

Tunamuomba Allaah Atukinge na ushirikina.

## Ni Mambo Gani Ambayo Raafidhwah Wametofautiana Na Ahlus-Sunnah?

Amesema Nidhwaamud-Diyn Muhammad Al-A`adhwamiy katika utangulizi wa kitabu chake *'Ash-Shiy´atu wal-Mut`ah'*: "Hakika tofauti zilizopo kati yetu na Ahlus-Sunnah si tofauti za kifiqhi peke yake, kama vile mas-alah ya Mut`ah n.k. - hapana, bali asili ya tofauti zetu ni katika mambo ambayo ndiyo misingi ya dini (Mambo ya kiitikadi) kama haya yafuatayo:

1. Raafidhwah wanadai kwamba Qur-aan imebadilishwa, hivyo ina mapungufu.

Na sisi tunasema: Hakika Qur-aan ni maneno ya Allaah yaliyotimia wala hayana mapungufu yoyote, hayakubadilishwa, wala hayatobadilishwa aidha kwa kupunguzwa au kuongezwa mpaka siku ya Qiyaamah. Kama alivyosema Allaah:

"Hakika Sisi Tumeuteremsha ukumbusho (Qur-aan), na hakika sisi Tutauhifadhi." [Al-Hijri: 9].

2. Raafidhwah wanadai kuwa Maswahaba wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) waliritadi baada ya kufa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) isipokuwa wachache tu, na wakafanya khiyana katika dini hasa hasa Makhalifa watatu; Abu Bakr, ´Umar na ´Uthmaan. Na kwa hiyo Makhalifa hawa watatu ni Makafiri na ni wapotofu kwa mujibu wa imani ya ki-Shia.

Na sisi tunasema: Hakika Maswahaba wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio viumbe bora baada ya Mitume, na kwamba wote ni waadilifu,

hawawezi kumsingizia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), na ni wakweli katika yale waliyoyanukuu kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

3. Raafidhwah wanadai kuwa: Hakika Maimamu wao kumi na mbili ni Ma'aswuwmiyn (wamehifadhiwa na madhambi), na kwamba wanajua ghayb na wanayo elimu yote waliyopewa Malaika, Manabii na Mitume, na kwamba wanajua mambo yote yaliyopita na yajayo, halifichikani kwao jambo lolote, na kwamba wao wanazijua lugha zote za ulimwenguni na kwamba dunia yote ni ya kwao.

Na sisi tunasema kwamba: Wao ni viumbe kama viumbe wengine, wamo miongoni mwao Wanavyuoni, na Makhalifa. Wala haifai kuwanasibisha na jambo ambalo wao hawakujinasibisha nalo bali wao walikataza mambo hayo na kujitenga mbali nayo kabisa. (76)

## Ni Ipi Itikadi Ya Raafidwah Kuhusu Siku Ya ´Aashuraa? Na Ina Ubora Gani Kwao?

Hakika Raafidhwah wanafanya mahafali na kuandamana mabarabarani na katika viwanja mbalimbali na kuomboleza na kuvaa mavazi meusi ili kuonyesha huzuni katika kukumbuka kifo cha Husayn (Radhiya Allaahu ´anhu) katika kumi la mwanzo la mwezi wa Muharram kila mwaka.

Wanafanya haya wakiitakidi kuwa jambo hili ni katika njia za kujikurubisha kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala), wanapiga mashavu yao na vifua vyao na migongo yao na kurarua nguo zao huku wakilia kwa makelele wakisema: Yaa Husayn..Yaa Husayn, bali hufikia wakajipiga kwa Minyororo na visu kama ilivyo katika nchi ambazo Raafidhwah ni wengi, kama Iran.

Na masheikh wao wanawahimiza sana katika mambo haya ambayo ni vichekesho kwa mtu mwenye akili timamu kuambiwa kwamba hii ni dini. Aliulizwa mmoja wa Mashaykh wao mwenye kutegemewa Muhammad

76 Utangulizi wa Nidhwaamud-Diyn Muhammad Al-´Aadhwamiy katika kitabu *'Ash-Shiy´atu wal-Mut`ah'* uk. 6.

Hassan Al-Kaashiful-Ghitwaa kuhusu mambo wanayoyafanya watu wake? Akasema: Hakika kufanya hivyo ni kuyaadhimisha matukufu ya Allaah kama ilivyokuja katika Suwratul-Hajj:

(Mwenye kuheshimu alama za (dini ya) Allaah, basi hilo ni jambo la uchaji wa nyoyo). [Al-Hajj: 32].

(Mambo haya ya kipuuzi Mashia wanayafanya kila mwaka. Na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekataza kujipiga mashavu na kuchana nguo…kwa huzuni ya kufiwa, kama ilivyokuja katika Hadiyth Swahiyh iliyopo katika Swahiyh Muslim Hadiyth nambari 103. Lakini Raafidhwah wao huzipiga ukutani Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa sababu wao ni miongoni mwa makundi yanayomkadhibisha Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

## Ni Ipi Itikadi Ya Raafidhwah Kuhusu Bay'ah (Kutoa Ahadi Ya Kumtii Mtawala)

Raafidhwah wanaitakidi kwamba kila utawala ambao si utawala wa Ithna-´Ashariyyah ni batili na haufai. Imekuja katika kitabu *'Al-Kaafiy Bisharhil-Maazindraaniy'* na katika *'Al-Ghaybah'* cha An-Nu'umaaniy kutoka kwa Abu Ja'afar amesema: "Kila Bendera itakayoinuliwa kabla ya Bendera ya Mahdi wa ki-Raafidhwah - basi mwenye kunyanyua bendera hiyo ni Twaaghuwt."[77]

Wala haifai kumtii mtawala ambaye hakuteuliwa na Allaah isipokuwa kwa misingi ya Taqiyyah, na kiongozi ambae ni jeuri na dhwaalimu ambaye hastahiki utawala haifai kumtii; wanawakusudia kwa sifa hizi watawala wote wa Kiislamu wasiokuwa katika Maimamu wao, na wa mwanzo kabisa katika watawala hao, ni Makhalifa wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) Abu Bakr, ´Umar, na ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anhum).

Amesema mmoja katika Raafidhwah, Al-Majlisiy ambaye ni mmoja katika wapotofu wao kasema katika kitabu chake *'Bihaarul-Anwaar'* kuhusu Makhalifa hawa watatu: "Hawakuwa ila ni waporaji tu, na ni watawala jeuri, walioritadi

[77] *Al-Kaafiy bisharh Al-Mazindraaniy* 12/371. Pia tazama *Al-Bihaar* 25/113.

kutoka katika dini, Allaah Awalaani na kila mwenye kuwafuata na kuwaunga mkono katika dhulma yao kwa Ahlul-Bayt."[(78)]

Haya ndio maneno ya kiongozi wao Al-Majlisiy ambaye kitabu chake ndio kitabu mama (chenye kutegemewa) katika Hadithi, haya ndio maneno yake kwa watu ambao ndio watu bora baada ya Mitume.

Na kutokana na mtazamo wao huu juu ya Makhalifa wa Waislamu basi wamemzingatia kila mwenye kuwakubali ni twaghuti na ni kiongozi jeuri. Amepokea Al-Kulayniy kutoka kwa ´Umar bin Handhwalah kuwa amesema: "Nilimuuliza Abu Abdillaah kwamba ikiwa watu wawili miongoni mwetu watakhtilafiana katika deni au Mirathi kasha wakapelekana kwa Qaadhwi au Hakimu jee inafaa? Akasema: Atakayetaka kuhukumiwa kwao katika misingi ya haki au batili, basi ajue anachukua haraam hata kama ni haki yake, kwa sababu atakuwa kaichukua kwa hukumu ya Hakimu ambaye ni Twaghuti."[(79)]

Amesema Al-Khumayniy (Khomeini) katika kitabu chake *'Al-Hukuwmatul-Islaamiyyah'* katika kuelezea mazungumzo yaliyotangulia hapo nyuma "Kiongozi mwenyewe anakataza watu kumuendea Qaadhwi, na analiona jambo hili ni kuwaendea Matwaghuti."[(80)]

Na imekuja katika kitabu *'At-Taqiyyatu fiy Fiqhi Ahlil-Bayt'* katika mlango wa tisa alipozungumzia Taqiyyah katika Jihaad, na maelezo yake haya ilikuwa ni kuunga mkono tafiti zilizofanywa na Mufti wao Ayattullaah Al-Haaj Muslim Ad-Daawry alipokuwa akielezea masharti ya kufanya kazi chini ya (mtawala) Dhwaalim - wanakusudia Mtawala yeyote ambaye ni katika Ahlus-Sunnah - akasema: "Hakika kufanya kazi chini ya Mtawala kumegawanyika sehemu tatu: (a) Kuna wakati inakuwa ni kwa nia ya kuwasaidia waumini wenzio. [(81)] na kusimamia maslahi yao, na kukidhi haja zao, kuingia kwa niyyah hii hukumu yake ni *mustahab* (inapendeza) na imehimizwa kufanya hivyo, (b) na mara nyingine inakuwa kwa niyyah ya kutafuta maisha na kujineemesha, kuingia kwa niyyah hii hukumu yake inajuzu japokuwa ni *makruhu* (haiimizwi mtu afanye hivyo) na endapo atawafanyia ihsani ndugu zake waumini na kukidhi haja zao hiyo itakuwa ni kafara kwake, kwa mujibu wa riwaya zilizokuja zikisharitisha hivyo. (c) na kuna wakati inakuwa ni kwa dharura na

---

78 *Al-Bihaar* cha Al-Majlisiy 4/385.

79 *Al-Kaafiy* cha Al-Kulayniy 1/67, *At-Tahdhiyb* 6/301, *Man Laa Yahdhwuruhul-Faqiyh* 3/5.

80 *Al-Hukuumatul-Islamiyyah* uk. 74.

81 Wanaposema waumini wanakusudia (Shia) kwa sababu Raafidhwah wanajiita Waumini.

haja ya kupata riziki (kula na kunywa) hukumu yake inakuwa ni halali na inajuzu bila chukizo lolote."[82]

Hebu tazama ndugu yangu Muislamu jinsi wanavyowahukumu Ahlus-Sunnah kuwa ni Madhwaalim na waovu!!

Na walivyojuzisha kufanya kazi na watawala wa ki-Sunni kwa masharti, ambayo miongoni mwayo ni kuwanufaisha Mashia, na hili liko wazi kabisa, maana huwezi kumkuta Shia katika nafasi fulani isipokuwa atajitahidi kadri awezavyo amuweke Shia mwenzake na kumuweka mbali kabisa Sunni.

Tunamuomba Allaah Awakinge Waislamu kutokana na shari zao.

## Ni Ipi Hukumu Ya Kujenga Mahusiano Na Ukaribu Kati Ya Ahlus-Sunnah Na Raafidhwah Washirikina?

Nitatosheka ndugu msomaji na kutaja makala moja tu miongoni mwa makala za Dr. Naaswir Al-Qifaariy katika kitabu chake *'Mas-alatut Taqriyb'* nayo ni makala ya saba, amesema - Allaah Amuhifadhi –:

"Inawezekanaje kujenga mahusiano na ukaribu na watu ambao wanakitoa kasoro Kitabu cha Allaah na kukifasiri kwa tafsiri zisizo sahihi, na wanadai kuwa Maimamu wao wameteremshiwa Vitabu baada ya Qur-aan,[83]na wanaona kuwa Al-Imaamah (Uimamu) ni Utume, na Maimamu wao ni kama Manabii au ni wabora kuliko Manabii, na wanaifasiri ibada ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) peke yake ambao ndio ujumbe waliokuja nao Mitume wote, kwa tafsiri zingine wazijuazo wao tu. Na wanadai kwamba Ibada ni

---

82 *Kitaabu At-Taqiyyah fiy Fiqhi Ahlil-Bayt* cha Shaykh Muslim Ad-Daawriy 2/153.

83 Tazama ndugu msomaji mwisho wa kitabu hiki moja kati ya Sura ambazo Raafidhwah wanadai kwamba zimeondolewa katika Qur-aan ambayo ni *'Suwrat Al-Wilaayah'* iliyonukuliwa katika kitabu *'Faswlul Khitwaab'* cha An-Nuuriy Atw-Twabraasiy, na huku ni kumkadhibisha Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) Ambae Kaahidi kukihifadhi Kitabu Chake, Aliposema: "Hakika Sisi Tumeuteremsha ukumbusho (Qur-aan) na hakika Sisi Tutauhifadhi" [Al-Hijr: 9].
Hivi mtu mwenye akili timamu anaweza kutia shaka juu ya ukafiri wa mwenye kuitakidi itikadi kama hizi?

kuwatii Maimamu, na kwamba Shirki ni kuchanganya Twaa ya Maimamu pamoja na wengine, na wanawakufurisha Maswahaba watukufu wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wanawahukumu Maswahaba wote kwamba waliritadi isipokuwa watatu au wanne au saba, kwa mujibu wa Riwaya zao tofauti tofauti, na wanatofautiana na Waislamu wote kiitikadi mbalimbali kama vile, itikadi ya Al-Imaamah, Al-'Iswmah, At-Taqiyyah n.k. na wana itikadi ya kufufuka Maimamu wao na Mashia wote…"[84]

## Ni Zipi Nukuu Za Salaf Na Khalaf Kuhusu Raafidhwah?

Amesema Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah):

"Wamekubaliana Wanavyuoni kwamba Raafidhwah ni kundi lenye kusema uongo, na uongo wao ni watangu".

Amesema Ash-hab bin ´Abdil-´Aziyz:

"Aliulizwa Maalik (Rahimahu Allaah) kuhusu Raafidhwah. Akasema: "Usiseme nao, wala usipokee kwao, kwa sababu ni waongo."

Na amesema Imaam Maalik (Rahimahu Allaah):

"Yeyote mwenye kuwatukana Maswahaba wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hana jina, au alisema hana fungu lolote katika Uislamu."

Na amesema Ibn Kathiyr katika kauli yake Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala):

"Muhammad ni Mtume wa Allaah. Na walio pamoja nae ni wenye nyoyo thabiti mbele ya Makafiri, na wenye kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu (pamoja), wakitafuta fadhila za Allaah na Radhi (Zake). Alama zao ziko katika nyuso zao kwa taathira (athari) ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurat. Na mfano wao katika Injili

[84] *Mas-alatut-Taqriyb* cha Shaykh Dr. Naaswir Al-Qifaariy 2/302.

(umetajwa hivi): kuwa (wao) ni kama mmea uliotoa matawi yake, kisha (matawi hayo) yakautia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawasawa juu ya kigogo chake ukawafurahisha walioupanda.".[Al-Fat-h: 29].

Akasema "Kutokana na riwaya hii Imaam Maalik (Rahimahu Allaah) katoa hukumu ya kuwa Raafidhwah ni Makafiri, wale wanaowakufurisha Maswahaba, akasema: "Kwa sababu wanawachukia Maswahaba, na mwenye kuwachukia ni kafiri kwa mujibu wa Aayah hii."

Amesema Al-Qurtwubiy:

"Kwa hakika kafanya vizuri Imaam Maalik katika makala yake haya na katika tafsiri yake hiyo yeyote atakayemdharau mmoja katika Maswahaba, au akamtuhumu yeyote katika riwaya zake basi atakuwa kamkanusha Allaah na kaibatilisha Shari´ah ya Kiislamu."(85)

Na amesema Abu Haatim:

"Ametusimulia Harmalah akasema: Nimemsikia Imaam Ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah) akisema: "Sijapata kumuona mtu mwenye kushuhudia uongo (waongo wakubwa) kuliko Raafidhwah."

Na amesema Muamal bin Uhaab:

"Nilimsikia Yaziyd bin Haaruwn akisema: Inafaa kupokea Hadiyth kutoka kwa mtu ambae ni *Mubtadi´i* (mzushi) kama atakuwa hawalinganii watu katu katika bid´ah zake, isipokuwa Raafidhwah haifai kupokea kwao kwa sababu ni waongo."

Na amesema Muhammad bin Sa'iyd Al-Aswbahaaniy:

"Nilimsikia Shariyk akisema: Chukua elimu kwa kila Mtu utakayekutana naye isipokuwa Raafidhwah usichukue kwake, kwa sababu wao hujiundia Hadiyth kisha wakaifanya kuwa ni katika dini."

85 Uswuwlu Madh-hab Ash-Shiy´ah Al-Imaamiyyah Al-Ithnaa-´Ashariyyah cha Dr. Naaswir Al-Qifaariy (3/1250)

Shariyk aliyetajwa hapo juu ni Shariyk bin ´Abdillaah, aliyekuwa Qaadhwi wa mji wa Kuufah.

Na amesema Muaawiyah:

"Nilimsikia Al-A'amash akisema: "Niliwadiriki watu, ambao walikuwa hawawatajwi ila kwa sifa ya uongo."

Anakusudia jamaa zake Mughiyra bin Sa'iyd Ar-Raafidhwiy - muongo mkubwa - kama alivyotajwa na Al-Imaam Adh-Dhahabiy.(86)

Na amesema Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) katika kuyaelezea waliyoyasema wema waliotangulia kuhusu Raafidhwah:

"Ama Raafidhwah asili ya bid´ah zao zinatokana na unafiki walionao pamoja na ukafiri, uongo kwao ni mwingi sana, na wao wanakiri hivyo, maana wanasema: Hakika dini yetu ni Taqiyyah, ambayo ni mtu kusema kwa ulimi kinyume na yale yaliyomo Moyoni na huu ndio Unafiki."(87)

Na amesema ´Abdullaah bin Ahmad bin Hanbal:

"Nilimuuliza Baba yangu kuhusu Raafidhwah, akasema: Ni wale wanaomtukana Abu Bakr na ´Umar." Na aliulizwa Imaam Ahmad kuhusu Abu Bakr na ´Umar, akasema: "Watakie Rahma na ujitenge mbali na kila mwenye kuwachukia." (88)

Na amepokea Al-Khallaal kutoka kwa Abu Bakr Al-Marwaziy, amesema:

"Nilimuuliza Abu ´Abdillaah kuhusu wanaomtukana Abu Bakr na ´Umar na bibi ´Aaishah, akasema: "Sioni kama yuko katika Uislamu mtu huyo."(89)

86 *Minhaajus-Sunnah* cha Shaykh-ul-Islaam bin Taymiyyah 1/59-60.
87 *Minhaajus-Sunnah* cha Shaykh-ul-Islaam bin Taymiyyah 1/68.
88 *Al-Masaail wa Rasaail Al-Marwiyatu 'an Ahmad bin Hanbal* cha ´Abdullaah bin Sulayman al-Ahmadiy 2/357.
89 *As-Sunnah* cha Al-Khallaal 3/493. Na hili ni tamko wazi toka kwa Imaam Ahmad kuhusu ukafiri wa Raafidhwah.

Na amepokea Al-Khallaal, amesema:

"Aliniambia Harb bin Ismaa'iyl Al-Karmaaniy, Amesema: Katuhadithia Muwsaa bin Haaruwn bin Ziyaad, Amesema: Nilimsikia Al-Faryabiy akiulizwa na mtu kuhusu hukumu ya mwenye kumtukana Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anhu), akasema: Ni kafiri, akasema: Inaruhusiwa kumswalia akifa? Akasema: Hapana."[(90)]

Na Ibn Hazm (Rahimahu Allaah) amesema kuhusu Raafidhwah pindi alipofanya mdahalo na Manaswara, wakamletea vitabu vya Raafidhwah ili wavitumie kujenga hoja:

"Hakika Raafidhwah si Waislamu, wala kauli zao si hoja katika Dini yetu, bali hilo ni kundi lililotokea baada ya kufa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa miaka 25, hilo ni kundi linalopita mapito ya Mayahudi na Manaswara katika ukadhibishaji na ukafiri."[(91)]

Na amesema Abu Zur'ah Ar-Raaziy:

"Pindi ukimuona mtu anamdharau na kumsema vibaya yeyote katika Maswahaba wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) basi tambua kuwa huyo ni mnafiki."

Na kiliulizwa kitengo cha Fat-wa cha Saudi Arabia 'Al-Lajnah Ad-Daa-imah':

Anasema muulizaji kuwa yeye na jamaa zake wanaishi jirani na markaz ya ki-Iraq, na kuna kundi la Madhehebu ya Ja'afariyyah (Mashia), wamo miongoni mwao waliokataa kula katika vichinjwa vyao, na wengine wakala, sasa swali letu ni kwamba, "Je, tunaruhusiwa kula katika vichinjwa vyao? Hali ya kuwa wao wanamuomba ´Aliy na Hasan na Husayn na wengineo wakati wanapokuwa na matatizo?

---

90 *As-Sunnah* cha Al-Khallaal 3/499.

91 *Al-Faswlu fil Milal wan Nihal* cha Ibn Hazm 2/78.

Kikajibu kitengo hicho kwa usimamizi wa Shaykh ´Abdul-´Aziyz bin Baaz, na Shaykh ´Abdur-Razzaq Al-´Afiyfiy, na Shaykh ´Abdullaah bin Ghudayyaan, na Shaykh ´Abdullaah bin Qu'uwd. Jawabu lao ni kama ifuatavyo:

"Kila sifa njema zinamstahiki Allaah peke Yake, na Rahma na amani zimfikie Mtume wetu pamoja na Maswahaba zake, amma ba'ad:

"Ikiwa hali ni kama alivyotaja muulizaji, kwamba watu anaoishi nao ni kundi la Ja'afariyyah, wanamuomba ´Aliy na Hasan na Husayn, basi ni washirikina na wametoka katika Uislamu, na hivyo haifai kula vichinjwa vyao kwa sababu ni mizoga, hata kama watataja jina la Allaah katika vichinjwa hivyo.[92]

Na aliulizwa Shaykh ´Abdullaah bin Al-Jibriyn swali, miongoni mwa maelezo aliyoyataja muulizaji:

Shaykh katika nchi yetu kuna jamaa mmoja ni Raafidhwah anafanya shughuli ya uchinjaji, hata Ahlus-Sunnah wanampelekea wanyama wao awachinjie, pia kuna baadhi ya mahoteli wananunua nyama kwake na kwa wengineo katika Raafidhwah wanaofanya kazi kama yake. Je, Shaykh, nini hukumu ya vichinjwa vyake? Je ni halali au ni haraam? Tunaomba fatwa yenu.

Akajibu Shaykh kama ifuatavyo:

Wa 'Alaykumus Salaam wa RahmatuLlaahi wa Barakaatuh. Haifai huyo Raafidhwah kuwachinjia wala kula vichinjwa vyake, kwa sababu wao ni washirikina, maana wanamuomba ´Aliy bin Abi Twaalib (Radhiya Allaahu ´anhu) wakati wa matatizo hata wakati wa raha, hata wanapokuwa 'Arafah na katika Twawaaf na Sa'ayi, pia wanawaomba watoto wake (Hasan na Husayn) na Maimamu wao, tumewasikia mara nyingi na hii ni shirki kubwa na ni kuritadi, na wanastahiki kuuawa.

Pia wanapetuka mipaka katika kumsifia ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhu) wanamsifu kwa sifa ambazo hazimstahiki yeyote isipokuwa Allaah, tumesikia mara nyingi katika viwanja vya ´Arafah, kwa vitendo hivi ni kwamba wametoka katika Uislamu (wameritadi) kwa sababu wamemfanya ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhu) ni Mola, na ndie mwenye kuuendesha ulimwengu na anajua ghayb, na sifa nyinginezo.

Pia wanaipinga Qur-aan, wanadai Maswahaba waliibadilisha na wakaondoa baadhi ya Aayah na Surah zinazowahusu Ahlul-Bayt, na maadui wa Ahlul-

[92] *Fataawa Al-Lajnah Ad-Daaimah Lil-Iftaa*, Mj. 2, uk. 264.

Bayt, na hivyo hawaifuati, wala hawaioni kama ni dalili. Vilevile wanawatukana na kuwataja vibaya Maswahaba wakubwa kama vile Makhalifa watatu, na Maswahaba kumi waliobashiriwa Pepo na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), pia wake zake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambao ni Mama wa Waumini, na Maswahaba mashuhuri kama Anas, Jaabir, Abu Hurayrah na wengineo, hawazikubali Hadiyth zao kwa sababu wanasema ni makafiri!! Wala hawazikubali Hadiyth zilizopo katika Swahiyh mbili (Al-Bukhaariy na Muslim) isipokuwa zinazowazungumzia Ahlul-Bayt, badala yake wanashikamana na Hadiyth za uongo ambazo hazina dalili yoyote juu ya madai yao, pia pamoja na hayo wao wanatumia unafiki kwa kusema kwa ndimi zao yaliyo tofauti na walioyaficha nyoyoni mwao, na wanasema:

"Asiyekuwa na Taqiyyah hana dini". Hivyo madai yao yakuwa ni ndugu zetu katika imani, na kwamba wanaipenda dini ni madai ya uongo yasiyokubalika.

Tunamuomba Allaah Atukinge na shari zao. Rahma na Amani zimfikie Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pamoja na Ahli zake na Maswahaba wake.[93]

## Suratul-Wilaayah Ambayo Wanadai Iliondolewa Katika Mus-haf

Imenukuliwa kutoka katika kitabu *'Faswlul-Khitwaab'*:

"Enyi mlioamini ziaminini nuru mbili tulizoziteremsha, zikikusomeeni Aayah zangu na kukutahadharisheni na adhabu ya siku kubwa. Nuru mbili hizi, moja yatokana na nyingine, na mimi ni mwenye kusikia na mjuzi. Hakika wale wanaotekeleza ahadi zao, pamoja na Mtume wake katika Aayah zangu wataingia katika Pepo yenye neema. Na wale waliokufuru baada ya kuamini kwao kwa kuzitenga ahadi zao, na yale aliyowataka Mtume wayafuate, basi watatupwa katika moto wa Jahiym. Walizidhulumu nafsi zao na wakamuasi yule aliyemuusia Mtume basi hao watanyweshwa motoni maji yachemkayo, hakika Allaah Ambae kaitia nuru mbingu na ardhi kwa Alivyotaka, na Akawachagua baadhi ya Malaika, na akajalia Waumini miongoni mwa viumbe wake, na Allaah Anafanya

[93] Fatwa hii ilitolewa na Shaykh baada ya kuulizwa swali kuhusu kushirikiana na Raafidhwah, ilikua ni mwaka 1414 H. Pia napenda kubainisha kuhusu maneno yasemwayo na baadhi ya watu kuwa Shaykh Jibriyn peke yake ndio kawakufurisha Raafidhwah, maneno haya si kweli, bali wema waliotangulia (Salafus-Swaalih) wote walilikufurisha kundi hili.

Ayatakayo, hakuna Mola mwengine isipokuwa Yeye, mwingi wa Rahma Mwenye kurehemu. Kwa hakika walifanya vitimbi waliokuwa kabla yao kwa Mitume wao, basi Allaah Akawatia mikononi kwa sababu ya vitimbi vyao, hakika ukamataji wangu ni mkali na wenye kuumiza. Hakika Allaah Aliwaangamiza watu wa ʻAad na Thamuwd kwa ajili ya yale waliyoyachuma, na Akawafanya ni mazingatio kwenu, je hamuogopi?. Na Fir'awn kamuangamiza kwa ujeuri wake kwa Muwsaa na ndugu yake Haaruwn, nikamzamisha baharini na wafuasi wake wote. Ili iwe ni mazingatio kwenu na hakika wengi wenu ni waovu. Hakika Allaah Atawajumuisha hiyo siku ya kukusanywa, hawataweza kujibu lolote pindi watakapoulizwa. Hakika moto wa Jahiymu ndio makazi yao na Allaah ni mjuzi mwenye hekima. Ee Mtume wafikishie uonyaji wangu, Hivi karibuni watajua. Kwa hakika wamepata hasara wale waliokuwa wakizipinga Aayah Zangu na hukumu Zangu. Mfano wa wale wanaotelekeza ahadi zao, hakika nitawalipa Pepo yenye neema. Hakika Allaah ni Mwenye Maghfira na malipo makubwa. Hakika ´Aliy ni katika wachaji Allaah. Na hakika Sisi tutampa haki yake siku ya Qiyaamah. Hatukuwa Sisi juu ya dhulma aliyofanyiwa ni wenye kughafilika. Na Tulimkirimu juu ya watu wako wote. Hakika yeye na kizazi chake ni wenye subira. Na hakika adui yao ni kiongozi wa waovu sema uwaambie waliokufuru baada ya imani yao mmetafuta mapambo ya dunia na mmeyafanyia haraka mkasahau Aliyokuahidini Allaah na Mtume Wake, na mkazitengua ahadi baada ya kuahidi kwenu, na tumekupigieni mfano huenda mkaongoka. Ee Mtume kwa hakika Tumekuteremshia dalili zenye kupambanua mna ndani yake kwamba atakayefishwa ilihali ni Muumin, na watakaomtii baada yao watadhihiri.

Basi jiepushe nao hakika wao wamekengeuka. Kwa hakika sisi Tutawahudhurisha, katika siku ambayo hakitawasaidia chochote wala hawatahurumiwa. Wataingia katika Jahannam makazi ambayo hawatoondolewa. Basi litukuze jina la Mola na uwe ni miongoni mwa wenye kusujudu. Hakika tulimpeleka Muwsaa na Haaruwn wakawakanusha. Wakavumilia juu ya kukadhibishwa huko. Tukawageuza wakadhibishaji kuwa Manyani na Nguruwe na tukawalaani mpaka siku ya Mwisho. Basi subiri hivi karibuni wataona. Kwa hakika Tumekupa hukumu kama zile Tulizowapa wale wa kabla yako miongoni mwa Mitume na tukakuchagulia miongoni mwao mteule ili wapate kurejea. Na yeyote atakayekengeuka amri yangu, basi kwangu ndio marejeo yake, Basi na wastarehe kidogo na ukafiri wao, wala usiulize kuhusu wale wenye kuvunja ahadi. Ee Mtume hakika tumeweka katika shingo za Waumini ahadi, basi ichukue na uwe miongoni mwa wenye kushukuru. Hakika ´Aliy ni mnyenyekevu, mwenye kusimama sana usiku akiogopa Aakhirah na kutaraji thawabu za Mola Wake, sema: Je, wako sawa

wale waliodhulumu hali ya kuwa wanazitambua adhabu Zangu? Tutaweka shingoni mwao makongwa, nao watajuta juu ya matendo yao. Hakika Sisi Tumekubashiria kizazi chake chema. Na wao hawatozikhalifu amri Zetu. Wanazo Rahma kutoka Kwangu katika uhai wao na katika kufa kwao, na siku ya kufufuliwa wale wanaowafanyia uadui baada yako wanazo ghadhabu Zangu, hakika hao ni watu waovu waliopata khasara. Na wale waliopita mapito yao wana Rahma toka kwangu nao watakuwa katika vyumba vya Peponi katika hali ya amani kabisa. Na shukurani zote zinamstahiki Allaah Mola wa walimwengu wote.(94)

## Lawh (Ubao) Wa Faatwimah Wanaodai Mashia

Hiki ni kitabu kutoka kwa Allaah Mtukufu Mwenye hekima kwa Muhammad Nabii Wake na nuru Yake na Mjumbe na dalili Yake, ambacho kateremka nacho Jibriyl kutoka kwa Allaah.

Ee Muhammad yatukuze majina Yangu, na uzishukuru neema Zangu, wala usikanushe utukufu Wangu, hakika mimi ndiye Mola wako hapana Mola wa haki ila Mimi, basi atakaetegemea fadhila zisizokuwa Zangu, au akaogopa usiokuwa uadilifu Wangu, basi Nitamuadhibu adhabu ambayoSsitomuadhibu yeyote katika walimwengu wote, basi Niabudu Mimi, na unitegemee Mimi tu, hakika Mimi Sijapata kumtuma Nabii yeyote akakamilisha masiku yake na kumaliza muda wake isipokuwa huwa ninamjalia Waswiy (mrithi), na Mimi Nimekufadhilisha juu ya Manabii wote na Nimemfadhilisha (mrithi wako) juu ya warithi wote, na Nimekukirimu kwa wajukuu zako wawili, nikamjalia Hasan kuwa ndio Madini ya elimu yangu baada ya kumalizika muda wa baba yake.
Na nikamjali Husayn kuwa ni hazina ya wahyi Wangu, na Nikamkirimu kwa kufa Shahiyd na Nikafanya mwisho wake ni mwema, yeye ni mbora wa mashahidi na mwenye daraja kubwa.

94 Hii ndio *Suwratul-Wilaayah* wanayodai Mashia, imenukuliwa kutoka katika kitabu *Faswlul-Khitwaab fiy Ithbaat Takhriyf Kitaab Rabil-Arbaab*, tumeamua kuiandika ili msomaji aweze kuona jinsi wanavyomkanusha Allaah Ambaye Kaahidi kukilinda Kitabu Chake kutokana na kubadilishwa.

Nikajaalia neno Langu na hoja Yangu Kwake, kwa sababu ya kizazi chake Ninaadhibu na kulipa mema, wa mwanzo wao ni ʻAliy ambae ni bwana wa Wachaji na pambo la wateule Wangu, na mwanae ni sawa na babu yake mwenye kusifiwa Muhammad Al-Baaqir.

Wataangamia wenye kutia shaka juu ya Ja'afar, Mwenye kumkanusha ni sawa na aliyenikanusha Mimi. Limekwishathibiti neno Langu kuwa Nitayakirimu makazi ya Ja'afar. Mwenye kubadilisha Aayah moja katika Kitabu Changu basi atakuwa kanizulia. Ole wao wazushi wakanushao, pindi ukimalizika muda wa Muwsaa mja Wangu na kipenzi Changu na mbora Wangu kwa ´Aliy (…)[95]; Atazikwa katika mji ambao kaujenga mja mwema, kandokando ya mtu mbaya kabisa katika viumbe Vyangu. Limekwishatimia neno Langu kwa Muhammad mwanae na Khalifa wake baada yake na mrithi wa elimu yake.

Yeye ndiye mrithi wa elimu Yangu na ndie hoja Yangu kwa viumbe Wangu, hata muamini mja yeyote isipokuwa nitayafanya makazi yake ni Peponi na nitampa nafasi ya uombezi wa watu sabini katika watu wa nyumbani kwake ambao wote walistahiki kuingia motoni, na nitampa mwisho mwema mwanae ´Aliy kipenzi Changu, na muaminifu juu ya wahyi (ufunuo) Wangu. Nitamtoa kwake mlinganiaji katika njia Yangu na mlinzi wa elimu Yangu Al-Hasan na nilikamilisha hilo kwa mwanae (…)[96]Rahma kwa walimwengu, atakuwa na ukamilifi wa Muwsaa na uzuri wa ´Iysaa na subira ya Ayyuwb, watadhalilishwa Mawalii wangu katika zama zake, na watauawa na kuchomwa moto, na watakuwa wenye khofu na uoga, ardhi itatapakaa damu yao, na kuenea hali ya hatari kwa wake zao hao ndio mawalii Wangu wa kweli, kupitia kwao Nitaondoa fitna, na kwao Nitaondoa matatizo na misukosuko, hao ndio wana Rahma na Amani kutoka kwa Mola wao na hao ndio wenye kuongoka.

Kasema: Abdur-Rahmaan bin Saalim: Amesema Abu Baswiyr: Lau kama hutosikia maisha yako yote isipokuwa Hadiyth hii basi inakutosha, hivyo ihifadhi isipokuwa kwa watu wake. [97] [98]

---

95 Hapa kuna ibara haikuwa wazi hivyo hatukuiandika ibara hiyo.

96 Kuna ibara ambayo haiko wazi ndio maana hatukuweza kuiandika.

97 Raafidhwah wanadai kuwa ubao wa Faatwimah alishuka nao Jibriyl (´Alayhis-Salaam) kwa Faatwimah (ʻAlayhas-Salaam) baada ya kufa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), na kwamba ʻAliy (Radhiya Allaahu ´anhu) wakati Jibriyl akishuka kwa Faatwimah alikuwa kajificha nyuma ya pazia akawa anaandika ayasemayo Jibriyl kumwambia Faatwimah (kama alivyoeleza Al-Kulayniyiy katika kitabu chake *Al-Kaafiy* 1/185-186 na huu ni uongo na uzushi mkubwa, maana wahyi ulikatika baada ya kufa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), pamoja na hayo ubao huo wanaoudai kwao ni sawa na Qur-aan Tukufu kwa Ahlus-Sunnah.

## Du'aa Ya Masanamu Wawili Wa Ki-Quraysh[99] Wanamkusudia Abu Bakr Na ´Umar (Allaah Awawiye Radhi)

Kwa jina la Allaah Mwingi wa Rahma Mwenye kurehemu.

Ee Allaah, mpe Rahma na amani Muhammad na watu wake, ee Allaah walaani masanamu wawili wa ki-Quraysh na matwaghuti wao na mabinti wao, ambao walikhalifu amri Yako, na wakaukanusha wahyi Wako, na wakazikanusha neema Zako, na wakamuasi Mtume Wako, na wakageuza dini Yako, na wakakibadilisha Kitabu Chako, na wakawapenda maadui Zako, na wakazipindisha hukumu Zako, na kuzigeuza Aayah Zako, na wakawafanyia uadui mawalii Wako, na wakauharibu mji Wako na kuwaharibu waja Wako.

Ee Allaah walaani, na wafuasi wao, na wenye kuwapenda, kwa hakika waliiharibu nyumba ya utume, na wakavunja mlango wake, na kuharibu sakafu yake, na kuwaondoa watu na wakauwa watoto wake, na wakaiepusha mimbari yake na mrithi wa elimu yake, na wakakanusha uimamu wake, na wakamshirikisha Mola wao, yakawa makubwa madhambi yao, na kwa hiyo wakawa ni watu wa kudumu motoni, na kipi kitakujulisha hiyo Saqar? Haibakishi wala haisazi.

Ee Allaah, walaani kwa idadi ya kila ovu walilolifanya, na kwa kila haki waliyoificha, na kwa kila mimbari walioipanda, na kwa kila mnafiki waliomtawalisha, na kwa kila waliomuudhi, na kwa kila mkweli waliyemfukuza, na kwa kila kafiri waliyemnusuru, na kila kiongozi waliyemtenza nguvu, na kila faradhi waliyoibadilisha, na kila athari waliyoibadilisha, na kila damu waliyoimwaga, na kwa kila kheri waliyoibadilisha, na kila ukafiri waliousimamisha, na kila haraam walioila na kila khumus waliojihalalishia na kila batili waliyoiasisi na kila unafiki waliouficha, na kila dhulma waliyoieneza, na kila amana waliyoifanyia khiyana, na kila ahadi waliyoivunja, na kila halali waliyoiharamisha, na haraam waliyoihalalisha, na kila mtukufu waliomdhalilisha, na kila dhalili waliomtukuza…

---

[98] *Al-Kaafiy* cha Al-Kulayniyiy 1/527, na *Al-Waafiy* cha Al-Faydhwu Al-Kaashraaniy, Mj. 1 2/72, na *Ikmaalud-Diyn* cha Ibn Baabawayhi Al-Qummiy uk.301-304, na *I'ilaamul-Waraa* cha Abu 'Aliy Atw-Twabrasiy uk. 152.

[99] Tumeamua kuichapa du´aa hii ambayo wanaiita du´aa ya masanamu wawili wa ki-Quraysh, ili msomaji aweze kuisoma ambayo wanamkusudia Abu Bakr na ´Umar na Bibi ´Aaishah na Bibi Hafswah (Allaah Awawiye radhi wote).

Ee Allaah, walaani kwa idadi ya kila Aayah waliyoibadilisha, na kila faradhi waliyoiacha, na kila Sunnah waliyoibadilisha, na kila hukumu waliyoivunja, na kila wasia walioubadilisha, na kila mambo waliyoyabadilisha, na mambo waliyoyapoteza, na kila shahada walizozificha na kila khiyana waliyoifanya.

Ee Allaah walaani katika siri na dhahiri, laana zilizokuwa nyingi kabisa, daima isiyo na kikomo, laana isiyomalizika, walaani wao na wasaidizi wao, na kila mwenye kuwapenda, na kila wenye kufuata maneno yao na wenye kuzisadikisha hukumu zao. (Kisha sema mara nne) Ee Allaah walaani wote, ewe Mola mpe Rahma Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pamoja na Ahli zake, nitosheleze kwa halali zako kutokana na haraam zako, na unikinge na ukafiri.

Ee Mola wangu hakika nimekosea na kuidhulumu nafsi yangu, ninakiri madhambi yangu na sasa niko mbele yako iweke nafsi yangu katika radhi zako, sitorejea, na kama nikirejea basi nisamehe, kwa fadhila na ukarimu wako, ee mwingi wa huruma. Rahma na amani zimfikie bwana wa Mitume na mwisho wa Manabii wote na Ahli zake watukufu, ee mwingi wa Rahma."[(100)]

## Hitimisho

Baada ya yote yaliyotangulia, bila shaka ndugu yangu Muislamu utakubaliana na mimi kwamba mwenye kuifuata dini hii potofu si miongoni mwa Waislamu hata kama yeye atajiita Muislamu, sasa nini wajibu wako wewe ndugu yangu Muislam juu ya hawa Raafidhwah (Mashia) hasa ukizingatia kuwa wanaishi na Waislamu na wanajinasibisha na Uislamu?

Wajibu wako ni kuchukua tahadhari nao, na kutoshirikiana nao na kuwatahadharisha watu kutokana na itikadi zao mbaya ambazo zimejengeka juu ya kumfanyia uadui kila mwenye kumpwekesha Allaah na kumuamini Allaah na Mtume wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Amesema Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah:

---

100 *Miftaahul-Jinaan* cha ʻAbbaas Al-Qummiy uk. 114.

"Ama Raafidhwah hawaishi na mtu yeyote isipokuwa katika misingi ya unafiki kwa sababu dini yao iliyomo nyoyoni mwao ni mbovu, inawafanya waishi katika misingi ya uongo na khiyana, na kuwafanyia watu ubaya, hawaachi shari yoyote walio na uwezo nayo isipokuwa huifanya. Na endapo wakiwa hawajulikani kwa watu kuwa ni Raafidhwah basi utaona nyusoni mwao alama za unafiki."[101]

Hakika wao wameficha chuki nyingi dhidi yetu, pamoja na hivyo utawaona baadhi ya watu katika Ahlus-Sunnah wenye kudanganyika nao wanashirikiana nao na kuwaamini sana, na yote hii ni kwa sababu ya kuwa mbali na Kitabu cha Allaah na kuyapa nyongo mafundisho ya Dini yetu na kutojua hukumu zake zinazomuamuru Muislamu kujiweka mbali na kila kafiri na mshirikina. Kwa maelezo haya bila shaka tutakuwa tumejua wajibu wetu kama waislamu.

Tunamuomba Allaah Ainusuri Dini Yake, na Alinyanyue Neno Lake, na Awadhalilishe Raafidhwah na wafuasi wao, na Awafanye kuwa ni ngawira kwa Waislamu. Rahma na amani zimuendee Mtume wetu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Ahli zake na Maswahaba zake wote.

**Imeandikwa na ‘Abdullaah bin Muhammad As-Salafiy.**

**Allaah Amsamehe yeye na wazazi wake na Waislamu wote.**

101 *Minhaajus-Sunnat An-Nabawiyyah* cha Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah 3/360.

## Rejea Muhimu Ambazo Tunamnasihi Kila Muislamu Kuzijua Katika Kuwajibu Raafidhwah

1- Fataawa Shaykh Al-Islaam Ibn Taymiyyah.

2- *Minhaajus-Sunnah* cha Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah.

3- *Al-Milal wan-Nihal* cha Ash-Shaharistaaniy.

4- *Al-Farqu baynal-Firaq* cha Al-Baghdaadiy.

5- *Maqaalatul-Islaamiyyiyn* cha Al-Ash'ariy

## Miongoni Mwa Vitabu Vya Wanavyuoni Wa Zama Hizi

1- Vitabu vyote vya Shaykh Ihsaan Ilaahi Dhwahiyr.

2- *Mas-alatu Taqriyb* cha Shaykh Dr. Naaswir Al-Qifaar.

3- *Uswuwl Madh-habu Ash-Shiy'ah Al-Ithnaa-'Aashariyyah* cha Shaykh Dr. Naaswir Al-Qifaar.

4- Vitabu vyote vya Shaykh Muhammad Maali-Llaah.

5- *Badhwlul-Majhuwd fiy Mushaabahat Ar-Raafidhwah lil Yahuwd* cha ´Abdullaah Al-Jaamiyly.

6- *Hattaa laa nan khadi´a* cha 'Abdullaah Al-Muwswiliy.

7- *Ash-Shiy'atul Ithnaa 'Ashariyyah wa Takfiyruhim li-'Umuwmil Muslimiyn* cha ´Abdullaah As-Salafiy.

8- *Man Qatalal-Husayn* cha ´Abdullaah bin ´Abdil-´Aziyz.

9- *Al-Burhaan fiy Tabri-at Abi Hurayrah minal-Buhtaan* cha 'Abdullaah An-Naaswir.

10- *Al-Intiswaar lisw-Swuhbi wal-Aal* cha Ibrahiym Ar-Rahiyliy.

11- *Kashful Jaaniy Muhammad At-Tijaaniy* cha Shaykh ´Uthmaan Al-Khamiys.

12- *Bal-Dhwalalta fiy Radd Abaatwiyl At-Tijaaniy* cha Shaykh Khaalid Al-'Asqalaaniy.

13- *Ma'a Al-Ithnaa 'Aashariyyah fil Uswuwl wal Furuw'* cha Dr. ´Aliy As-Saaluws.

14- *Tabdiyd Adhw-Dhwalaam wa Tambiyh An-Niyaam ´alaa Khatwari Tashayyui ´alal Muslimiyn wal-Islaam* cha Shaykh Sulaymaan Al-Jabhaan.

Na vingine vingi. Hapa tumefupisha tu.

**Tovuti Muhimu Za Kuwajibu Raafidhwah Ithnaa-´Ashariyyah, Ambazo Tunakusihi Uzitembelee**

1- http://www.dd-sunnah.net

2- http://www.fnoor.com

3- http://www.albrhan.com

4- http://www.wylsh.com

5- http://www.khomainy.com

6- http://www.dhr12.com

7- http://www.albainah.net

8- http://www.ansar.org

9- http://www.almanhaj.com

10- http://www.isl.org.uk

11- http://www.almhdi.com